

UKURASA 20

**Abdu Kiba apata kigugumizi**

## Majaliwa apigia chapuo kilimo cha bustani



WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema...

UKURASA 4

**MAISHA**

Desemba 6, 2020 Nipashe — Baba, Mama na Mwana — *Jumapili*



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**
Jinsi ya kusafisha sofa lenye kitambaa



**HARUSI**

Ukurasa 12



**Namna ya kuandaa soseji ya mboga**

Ukurasa 14



'BULL RING'
**Pete ya pua inayompamba mwanamke**

Ukurasa 14


# Nipashe JUMAPILI

Jumapili Desemba 6, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • No. 0580421


## BARAZA LA MAWAZIRI:

# VIGOGO WATEMWA

**SURA** mpya zatawala, vijana washamiri unaibu waziri...

*Endelea uk. 2*

### WALIOTEMWA



Hamisi Kigwangala




Isack Kamwelwe



Japhet Hasunga




Luhaga Mpina



Mussa Azzan 'Zungu'

### SURA MPYA



Dk. Doroth Gwajima



Dk. Leonard Chamuriho



Godfrey Mwambe



Mashimba Mashauri Ndaki



Prof. Adolf Mkenda



Prof. Kitila Mkumbo

## Asimulia alivyopata VVU siku harusi ya rafiki yake

UKURASA 2

## BIBI ADAIWA KUMUUNGUZA MJUKUU KISA KACHANA SHUKA

UKURASA 3

**MICHEZO** KIPA WA BIASHARA ANUKIA AZAM FC UK. 23

# Asimulia alivyopata VVU siku ya harusi ya rafiki yake

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa jijini Dar es Salaam, Veronica Lyimo, amesimulia harusi ya rafiki yake ilivyobadili maisha yake baada ya kushiriki tendo la ndoa bila kinga kwa mara ya kwanza na kupata maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU).

Akihojiwa katika kipindi cha MamaMia kinachoruka kila siku Jumatatu hadi Ijumaa na East Africa Radio, Lyimo alisema kuwa baada ya kujigundua ana maambukizi alilazwa wodi ya vichaa kwa miezi mitatu.

Akisimulia zaidi mkasa huo, alisema alipima VVU kwa mara ya kwanza mwaka 2015 katika maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani.

Lyimo alisema aliamua kupima afya ili kujua kama ana maambukizi ya VVU au la na baada ya kupima, vilikuwa havisomi vizuri na kuambiwa majibu yake ni tata.

"Mwisho wa siku walinitaka niende hospitali kubwa ili kupata majibu zaidi. nilikwenda Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) na nilipopima majibu yalionyesha nina maambukizi ya virusi vya Ukimwi," alisema. Lyimo alisema wakati akipima Muhimbili, baba yake mzazi alikuwa amelazwa hospitalini hapo na matokeo aliyoyapata hakuridhika nayo. "Mimi ni mtoto wa kwanza kwenye familia na mbaya zaidi ndugu zangu wananitegemea na wengine walikuwa wanasoma kwa hiyo macho yote yalikuwa yananiangalia. Veronica alisema baada ya majibu aliyopewa Muhimbili, aliamua kumweleza mwenzi wake ambaye alishiriki nae tendo la ndoa, lakini kinyume cha matarajio, hakulipokea kwa mshtuko.


"Mwisho wa siku nikagundua kwamba alikuwa anatoa maambukizi yake na hana mwamko na alikuwa amedhamiria. Mtoto wangu hana maambukizi.

"Baada ya kugundua hili, niliondoka katika nyumba tuliyokuwa tunaishi na kurudi nyumbani. Nilimshirikisha mdogo wangu wa tatu wa kiume na alipokea vizuri, aliniambia huo si mwisho wa kuishi kuna maisha baada ya maambukizi," alisema. Lyimo alisema alimshirikisha mdogo wake huyo pekee kwa sababu wengine walikuwa bado wadogo na wakati huo walikuwa kwenye kipindi kigumu cha kumpoteza mama yao mzazi.

"Kukubali majibu ilinichukua muda kidogo maana ilifika hatua nililazwa wodi ya vichaa kwa sababu nilipata msongo wa mawazo. Nililazwa miezi mitatu na aliyekuwa akiniangalia kwa ukaribu alikuwa mjomba wangu.

"Baada ya kuruhusiwa mjomba alinichukua na kuanza kunipa ushauri nasaha na baadaye aliniingiza kwenye makundi ya wanawake wanaoishi na virusi vya Ukimwi, kunikutanisha na klabu za vijana na huko ndiko nilikojengewa uwezo kuona wako watu wanaishi na maambukizi na wana afya nzuri," alisema.

Kwa miaka mitatu ya mwanzo baada ya kukutana na mwenza wake, alisema walikuwa wakitumia kinga



na mwisho wa siku kitendo kimoja walichofanya bila kinga ndicho kilichomsababishia kupata maambukizi.

"Ninakumbuka siku hiyo tulikuwa wote tumetoka kwenye harusi ya rafiki yetu na usiku huo ndio tulilala bila kutumia kinga. Kiliniumiza kwa sababu kipindi chote niliweza kujilinda, lakini usiku mmoja ndio ulinifanya hivi nilivyo sasa," alisema.



Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, akitanga Baraza la Mawaziri, lililoundwa na Rais Dk. John Magufuli, Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA NA IKULU**

# Vigogo watemwa Baraza la Mawaziri

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli, jana alitangaza Baraza la Mawaziri 23 na manaibu wao huku baadhi ya vigogo waliokuwa katika baraza lililopita wakitemwa na sura mpya, wakiwamo vijana, zikichomoza.

Katika baraza hilo lililotangazwa na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma, Rais pia ameunda Wizara mpya ya Mawasiliano na Taknolojia ya Habari, huku Dk. Faustine Ndugulile akiteuliwa kuiongoza.

Sambamba na wizara mpya, Rais pia ameweteua waliokuwa makatibu wakuu wawili wa wizara kuwa wabunge na mawaziri. Walioteuliwa na wizara zao kwenye mabano ni Dk. Dorothy Gwajimba (Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto) na Dk. Leonard Chamuriho (Ujenzi na Uchukuzi). Kabla ya hapo, Dk. Gwajima alikuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Afya na Dk. Chamuriho alikuwa Katibu Mkuu iliyokuwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**WALIOTEMWA**

Mawaziri wa zamani waliotemwa katika baraza jipya na wizara zao kwenye mabano ni Mussa Zungu (Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira), Dk. Hamis Kigwangallah (Maliasili na Utalii), Japhet Hasunga (Kilimo), Luhaga Mpina (Mifugo na Uvuvi), Isack Kamwelwe (Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano).

Pia katika orodha yawalioachwa, wamo waliokuwa naibu mawaziri. Baadhi ya waliotemwa katika safu mpya ni Mhandisi Stella Manyanya (Viwanda na Biashara), Mussa Sima (Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira), Joseph Kandege (TAMISEMI) na Atashasta Nditiye (Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano).

Wengine ni Subira Mgalu (Nishati), Juliana Shonza (Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo), Dk. Ashatu Kijaji (Fedha na Mipango), Stela Ikupa (Ofisi ya Waziri Mkuu, wenye Ulemavu), Antony Mavunde (Ofisi ya Waziri Mkuu, Vijana na Ajira) na Constantine Kanyasu (Maliasili na Utalii).

**SURA MPYA**

Katika safu ya baraza jipya la mawaziri, ziko sura mpya ambao ni Prof. Kitilla Mkumbo (Ofisi ya Rais, Uwekezaji), Mashimba Ndaki (Mifugo na Uvuvi), Pro. Adolph Mkenda (Kilimo), Geoffrey Mwambe (Viwanda na Biashara).

**WABAKI PALE PALE**

Baadhi ya mawaziri wameendelea katika wizara walizokuwa wakiziongoza katika baraza lililopita. Mawaziri hao ni William Lukuvi (Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi), Kapteni mstaafu George Mkuchuka (Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), Prof. Joyce Ndalichako (Elimu, Sayansi na Teknolojia) na Doto Biteko (Madini).

Wengine ni Dk. Merdard Kalemani (Nishati), Selemani Jafo (Ofisi ya Rais - TAMISEMI), George Simbachawene (Mambo ya Ndani ya Nchi), Dk. Mwigulu Nchemba (Katiba na Sheria), Dk. Philip Mpango (Fedha na Mipango) na Prof. Palagamba Kabudi (Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki).

Naibu Mawaziri waliobaki katika wizara zao ni Dk. Angeline Mabula (Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi), Dk. Godwin Mollel (Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto) na Hussein Bashe (Kilimo).

**WAPANDA, WABADILISHWA WIZARA**

Rais katika baraza jipya pia amewapandisha waliokuwa mawaziri kwenye baraza lililopita na kuwapa nafasi mpya. Waliopandishwa ni Jumaa Aweso (Maji) na Dk. Damas Ndumbaro (Maliasili na Utalii) kabla ya hapo Aweso alikuwa Naibu Waziri wa Maji na Dk. Ndumbaro alikuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mwingine aliyepanda ni Elias Kwandikwa ambaye anakuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kabla ya hapo alikuwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano anayeshughulikia Ujenzi na Uchukuzi.

Sambamba na waliopandishwa, Rais Magufuli amemhamisha Ummy Mwalimu kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwenda Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira. Mwingine aliyehamishwa ni Innocent Bashungwa kutoka Viwanda na Biashara kwenda Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Kwa upande wa naibu mawaziri, waliohamishwa ni Abdallah Ulega kutoka Mifugo na Uvuvi kwenda Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; Mwita Waitara (TAMISEMI kwenda Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira) na William ole Nasha (Elimu, Sayansi na Teknolojia kwenda Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki).

**NAIBU MAWAZIRI WAPYA**

Naibu Mawaziri wapya walioteuliwa ni Geoffrey Pinda (Katiba na Sheria), Patrobas Katambi (Waziri Mkuu, Kazi na Ajira), Khamis Hamza Hamis (Mambo ya Ndani ya Nchi), Pauline Gekul (Mifugo na Uvuvi), Deogratius Ndejembi (Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) na Mmwanadidi Ali Khamis (Fedha na Mipango).

Wengine ni Omary Kipanga (Elimu, Sayansi na Teknolojia), Dk. Festo Lugange (TAMISEMI), Stephen Byanato (Nishati), Matthew Kundo (Mawasiliano na Teknolojia ya Habari) Ndulane Kumba (Madini), Mhandisi Msongwe Kasekenya (Ujenzi), Ummy Nderiananga (Ofisi ya Waziri Mkuu wenye Ulemavu), Mhandisi Maryprisca Mahundi (Maji) na Mary Masanja (Maliasili na Utalii).

HABARI KITAIFA

## Ajali ya bodaboda yaua watatu Muheza

**Na Steven William,** MUHEZA

WATU watatu wamefariki dunia na wengine wawili kujeruhiwa Muheza mkoani Tanga, katika ajali ya pikipiki.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Tanga, Leopold Fungu, alisema jana kuwa ajali hiyo ilitokea katika eneo la Msangazi barabara ya kutoka Muheza Mjini kwenda Tarafa ya Amani baada ya pikipiki za abiria, maarufu kama bodaboda kugongana.

Fungu aliwataja walipoteza maisha kuwa ni Yohana Ndede (25) mkazi wa kijiji cha Mkanyageni ambaye alikuwa ni dereva wa pikipiki na Joshua Martine (16) mkazi wa kijiji cha Masimbani ambaye alikuwa ni mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Muheza.

Alimtaja mwingine kuwa ni dereva wa pikipiki iliyopata ajali, Hamisi Cosmas (20), mkazi wa kijiji cha Tingeni.

Kamanda Fungu alisema miili ya watu hao imehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya Muheza.

Pia aliwataja majeruhi kuwa ni Salehe Ramadhani mkazi wa Kijiji cha Mkanyageni na Abdallah Mzee, ambao wamelazwa katika Hospitali ya Wilaya Muheza.

Kamanda Fungu alisema chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi wa pikipiki waliyokuwa wanaendesha pamoja na kutokuvaa kofia ngumu.

# Adaiwa kumuunguza mjukuu kwa pasi kisa kachana shuka

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

MWANAFUNZI wa darasa la pili katika Shule ya Msingi Chiringe B, Bunda mkoani Mara, (jina limehifadhiwa), amejeruhiwa mwilini kwa kuchomwa na pasi na bibi yake kwa madai alichana shuka alilokuwa amejifunika.

Kutokana na masahibu hayo, mtoto huyo amechukuliwa na kituo cha kulelea watoto cha Nyumba Salama kwa ajili ya malezi na usalama wake.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Saranga, Philip Safari, na Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kabarimu, William Magabo, walithibitisha jana kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa mhusika wa tukio hilo ni Juliana Matutu, maarufu kwa jina la Mama Njara.

Akisimulia mkasa huo, Safari alisema baada ya mwanamke huyo kufanya kitendo hicho, alitokomea kusikojulikana na hadi sasa hajulikani mahali alipo.

Alisema baada ya kutenda tukio hilo, alimtelekeza mtoto huyo nyumbani bila huduma zozote na kumwacha akitahabika kwa maumivu.

"Kwa mujibu ya majirani wa mwanamke huyo, baada ya kumaliza kufanya ukatili huo, alisema kwamba anakwenda kusalimia msibani, lakini hadi sasa hajulikana alipo," alisema Safari.

Safari aliyataja maeneo ambayo mtoto huyo aliunguzwa kuwa ni kichwani, miguuni, mikononi na tumboni.

Alisema tukio hilo lilitokea mwishoni mwa wiki iliyopita na kwamba baada ya wanafunzi huyo kwenda shuleni, mwalimu aliyekuwa anasimamia mtihani wa darasa la pili, alimwona akitaabika, ndipo akamfuata na kumuuliza kinachomsibu.

Baada ya mwalimu huyo kumuuliza, mwanafunzi huyo alieleza mkasa uliomsibu pamoja na kumwonyesha majeraha.

Ofisa Mtendaji Magabo, alisema baada ya kusimulia mkasa uliomkuta, walimu walimchukua mwanafunzi huyo na kumpeleka katika ofisi ya mtaa.

Alisema taarifa ilitolewa kituo cha polisi kisha alipelekwa kwenye kituo cha afya cha mjini Bunda, ambako alitibiwa na kuruhusiwa.

Alisema kwa sasa mwanafunzi huyo anaishi naye nyumbani kwake, baada ya kukabidhiwa na walimu.

Alisema ameshazungumza na Mkurugenzi wa kituo cha kulea na kutunza watoto cha Nyumba Salama, Robhi Samwel, amekubali kumchukua moto huyo, ili kulelewa kituoni hapo.

Kwa upande wake, mtoto huyo alisema chanzo cha kufanyiwa ukatili huo ni kuchanika kwa shuka alilojifunika, ambalo lilikuwa na tundu kubwa katikati kutokana na uchakavu.



Wananchi wakipita katika barabara iliyoharibika kutokana na mvua inayoendelea kunyesha, katika eneo la Mbezi Makabe, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mageuzi mabasi mwendokasi ya gesi yaja

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya utengenezaji mabasi yanayotumia nishati jadidifu ya gesi ya ETEFA kutoka Austria, imeonyesha nia ya kuwekeza katika mabasi ya mwendokasi kwa kuleta mabasi yanayotumia gesi badala ya mafuta.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana katika kikao na Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DARTO, Mtendaji Mkuu wa Kampuni hiyo, Johann Rieger, alisema kampuni yake ina uzoefu wa kutosha wa kutengeneza mabasi ambayo hayatumii mafuta, jambo ambalo ni rafiki wa mazingira na pia linasaidia kupunguza gharama za uendeshaji.

"Mabasi tunayotengeneza yanatumia gesi na nimeelezwa kuwa Tanzania mnayo gesi ya kutosha, hivyo ni fursa kwenu kutumia rasilimali hiyo kwa ajili ya kuendeshea mabasi yaendayo kasi kwani kutumia gesi kunapunguza gharama za uendeshaji kutokana na matumizi ya mafuta kuwa ghali," Alisema Rieger.

Alisema endapo watapata fursa ya kuwekeza nchini katika mabasi ya mwendokasi, DART itakuwa mdau wa kwanza nchini kutumia huduma hiyo na itakuwa fursa kwa nchi zingine kuja kujifunza.

Mtendaji Mkuu alisema Tanzania kijiografia imekaa eneo zuri katika nchi za Afrika Mashariki na Kati, hivyo ikianzisha kitu chochote ni rahisi kuenea kwa urahisi na kwa haraka katika nchi zingine zinazoizunguka.

Kutokana na hali hiyo, alisema kama itaanza kutumia gesi asilia kwenye mabasi, itapata faida kubwa kwa kuwa itauza gesi na ajira zitaongezeka.

Mkurugenzi wa Fedha na Maendeleo ya Biashara wa DART, Susan Chaula, alisema wamepokea wazo la wawekezaji hao na watalifanyia kazi kwa kuwa kwa sasa Tanzania ina rasilimali ya kutosha ya gesi asilia ambayo ikitumika katika mabasi ya mwendokasi, itasaidia kupunguza gharama za uendeshaji pamoja na kutunza mazingira.

"Tumewapokea na tumewasikiliza. Kimsingi wana teknolojia ya kisasa kabisa kama walivyotuonyesha na kama watafanikiwa kuwekeza nchini, si tu tutapata faida ya kutumia gesi asilia tuliyo nayo, bali tutakuwa mfano duniani kwa kutumia nishati mbadala ambayo ni rafiki wa mazingira kama dunia inavyojielekeza kwa sasa," alisema.

Chaula aliwataka wawekezaji wengine watakaoona fursa za kuwekeza nchini, wasisite kuja kwa kuwa hata Rais John Magufuli amekuwa akisisitiza mara kwa mara kuwa wawekezaji wakaribishwe na wapewe ushirikiano wa kutosha kwa kwa sababu Tanzania ni mahali salama pa kuwekeza.

Kampuni ya ETEFA yenye makao yake makuu Vienna, Austria, inasifika duniani kwa teknolojia inayolinda na kuhifadhi mazingira na ni miongoni mwa kampuni chache zilizowahi kushinda tuzo za kimataifa za uhifadhi wa mazingira.

# Majaliwa apigia chapuo kilimo cha bustani

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema tasnia ya kilimo cha mazao ya bustani ina mchango mkubwa kwenye maendeleo ya uchumi nchini na kuajiri watu zaidi ya milioni nne, hivyo kuongeza kipato kwa wakulima na wafanyabiashara.

Kutokana na umuhimu wa tasnia hiyo, Majaliwa ameiagiza Wizara ya Kilimo kuanzisha Mamlaka ya Kilimo cha Mazao ya Bustani na Kituo cha Utafiti kwa ajili ya kusimamia na kuratibu mazao ya matunda, viungo na mboga.

Majaliwa alisema hayo jana baada ya kufungua Kongamano la Kikanda la Biashara la Uwekezaji katika Tasnia ya Mazao ya Bustani lililofanyika kwenye Hoteli ya Kilimanjaro Hyatt Regency, jijiji Dar es Salaam.

"Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita uzalishaji wa mazao ya bustani nchini uliongezeka kwa asilimia 10.5 kutoka tani 5,931,900 mwaka 2015/16 hadi kufikia tani 6,556,102 mwaka 2018/19," alisema.

Takwimu hizo, alisema zinathibitisha ukuaji wa tasnia hiyo na uwapo wa haja ya kuweka mikakati ya kuiendeleza zaidi.

"Kwa kuwa bei kwa tani inakadiriwa kuwa Sh. 500,000 thamani ya mazao ya kilimo cha mazao ya bustani kwa mwaka 2018/19 inakadiriwa kuwa Sh. trilioni 3.3," alibainisha.

Waziri Mkuu alisema mbali na kuchangia katika ukuaji wa uchumi, tasnia hiyo inasaidia kujenga taifa lenye watu wenye afya nzuri, nguvu na uwezo wa kufanya kazi. Pia ni chanzo kikuu cha lishe na afya bora kwa Watanzania kutokana na virutubisho vingi kwa ulaji wa mboga, matunda na viungo.

Mazao ya bustani, alisema yamekuwa na mchango mkubwa katika kupambana na corona kwa sababu dawa mbadala za asili zilizosaidia wananchi wengi duniani kote kudhibiti ugonjwa huo, zilitokana na matunda na viungo.

"Kutokana na vilelezo hivyo, ni wazi kuwa mchango wa tasnia ya kilimo cha mazao ya bustani kwenye maendeleo ya watu na uchumi wa nchi yetu na dunia kwa ujumla ni mkubwa na iwapo fursa zilizopo zitafanyiwa kazi, basi safari yetu ya kuelekea kwenye uchumi ulio imara zaidi itakuwa ya mafanikio makubwa, kwa kipindi kifupi, " alisema.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu alisema katika kuimarisha miundombinu ya usafirishaji ili kuwezesha biashara hususon ya mazao yanayoharibika haraka kama mazao ya bustani, minofu ya samaki na nyama, serikali imepanga kununua ndege ya mizigo kwa kuzingatia mahitaji ya biashara na ukuaji wa uchumi.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, alisema kutokana na umuhimu wa tasnia hiyo, serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa zao hilo wameendelea kufanya uchambuzi wa athari za wadudu kwa ajili ya baadhi ya masoko mapya kama China, India na Afrika Kusini.

Pia alisema kutokana na umuhimu wa tasnia hiyo, serikali itaendelea kushirikiana na wadau kuzipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya kilimo ili iendelee kutoa mchango mkubwa katika taifa.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi Kilele ya Kilimo cha Maua, Mboga, Matunda na Viungo (TAHA), Jacqueline Mkindi (kulia), wakati wa mkutano wa kanda wa uwekezaji katika sekta ya mazao ya bustani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mil. 700/- zatolewa mikopo vikundi 72

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

HALMASHAURI ya Mji wa Njombe mkoani Njombe imetoa Sh. milioni 700 kwa vikundi 72 kwa ajili ya mkopo.

Akizungunza wakati wa kusoma taarifa ya fedha, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri hiyo, Enembora Lema, alisema kila mwaka halmashauri imekuwa ikitoa mikopo kama sheria inavyoelekeza.

"Fedha hizi zinatolewa kila robo kwa kutegemea makusanyo, hivyo leo tutakabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 7.9 kwa vikundi vya kiuchumi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu," alisema Lema.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Mhandisi Marwa Rubirya, alimtaka Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo na Idara ya Maendeleo ya Jamii kuhakikisha anafuatilia matumizi ya fedha hizo, kama zinatumika zilivyokusudiwa.

"Mikopo hii itumike kwa malengo yaliyokusudiwa, msije mkachukua fedha hizi kama vikundi mnafika kule mnagawana kununua baiskeli na mwingine analipa ada ya watoto, siyo lengo ya mikopo hii," alisema Rubirya na kuongeza:

"Nikuagize Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii mfuatilie vikundi hivi kuhakikisha shughuli zilizolengwa kufanyika ndizo zinazofanyika."

Mmoja wa wanakikundi toka kundi la wanawake, Deodata Mlowe, aliahidi kwenda kuzifanyia kazi fedha hizo kadri ya malengo yao, kwamba hawatazifuja kwa matumizi mengine.

# Malipo sadaka Sabato sasa kwa mtandao

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KANISA la Waadventista Wasabato kwa kushirikiana na Benki ya CRDB wamezindua mfumo utakaotumika kudhibiti mapato ya kanisa.

Mfumo huo utatumika kukusanya sadaka, zaka na michango mingine kwa kutumia benki na kampuni za simu zilizopo nchini.

Akizungumza jijini jana Dodoma wakati wa uzinduzi wa mfumo huo, Mkuu wa Idara ya Biashara kutoka Benki ya CRDB, Dk. Joseph Witts, alisema kwa kutumia benki hiyo na mitandao ya simu washiriki watatoa sadaka, zaka na michango mingine.

Dk. Witts alisema mfumo huo wa usimamizi wa fedha za kanisa utasaidia pia katika ukusanyaji wa mapato ya kanisa hilo, kwa kuwa tayari umeonyesha mafanikio makubwa katika taasisi nyingi ikiwamo Hospitali za Bugando na KMC.

"Niwapongeze Kanisa kwa uamuzi huu, maana licha ya kwamba katika kanisa kuna watu wametakaswa mmeamua kuja na mfumo wa kuzuia upotevu wa fedha kanisani. Nasema hongereni sana, mmetupa heshima kwani nchini kuna benki zaidi ya 50, lakini mmeamua kuja kwetu," alisema Dk. Witts.

Mkuu huyo alisema watausimamia mfumo huo na kuhakikisha kuwa unaleta mageuzi makubwa katika kanisa hilo.

Mchungaji Mkuu wa Kanisa la Waadventista wa Sabato, Jimbo la Kusini mwa Tanzania, Mark Malekana, alisema matarajio yao kupitia mfumo huo waumini watakuwa na imani ya kutoa matoleo, hivyo kuongeza uchumi wa kanisa.

"Kwanza mapato yataongezeka na yatakuwa salama na fedha hazitaibiwa kwani zikifika benki zinakuwa katika mikono salama, pia tunakuwa tupo katika matumizi ya teknolojia," alisema Askofu Malekana.

Mhazini Mkuu wa Kanisa hilo Jimbo la Kusini, Athanas Sigoma, alisema mfumo huo umeanzishwa ukiwa na malengo makubwa kwa kutumia mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Alisema kutokana na ukubwa wa kanisa hilo awali wahasibu walikuwa wakisafiri kwenda maeneo mbalimbali kwa ajili ya kukusanya sadaka wakiwa na vitabu vya risiti, lakini baada ya mfumo huo wanaamini utaokoa fedha nyingi walizokuwa wakizitumia.

Alisema: "Tuna zaidi ya makanisa 4,000, wahasibu kila siku walikuwa wanasafiri kwenda maeneo mbalimbali, hivyo kwa sasa gharama zinapungua kwani wengi watalipa kwa njia ya simu tu kwa kutumia mitandao ya simu."

## HABARI KITAIFA

# RC aomba msaada malezi ya yatima

**Na Mwandishi Wetu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, amewaomba wadau kujitokeza kuwasaidia watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu.

Alitoa rai hiyo jana wakati akikabidhi msaada wa tani 1.7 za mchele ukiwa na thamani ya Sh. milioni 3.1 kwa vituo vya kulea watoto yatima mkoani Shinyanga.

"Wakati wa mlipuko wa ugonjwa wa corona watu wengi waliokuwa wanasaidia watoto yatima walisitisha kutoa huduma, sisi kama mkoa tukaona tuangalie namna ya kusaidia ili watoto hawa waendelee kuishi," alisema.

"Naomba wadau wajitolee ili kusaidia watoto hawa waweze kuishi na kuendelea kusoma wakiwa na mahitaji ya vifaa vya shule," aliongeza.

Telack alisema mkoa wa Shinyanga una vituo vingi vya kulelea watoto ikiwamo Shirika lisilo la Kiserikali la Agape ACP ambalo tayari lishapewa msaada wa vyakula, pamoja na kituo cha Shinyanga Society Orphanage Centre kinacholea watoto wasio na wazazi.

Akipokea msaada huo kwa niaba ya vituo vya kulelea watoto yatima, Mkurugenzi na Mwanzilishi wa Shinyanga Society Orphanage, Ayam Said, alimshukuru mkuu huyo wa mkoa kwa ushirikiano anaoendelea kuwapatia.

Alisema licha ya kupewa msaada wa chakula, lakini bado wanahitaji msaada wa zana za kufanyia kazi ili watoto wafanye kazi, wawe watoto bora na baadaye kuwa wafanyakazi bora wa serikali.

Aliongeza kuwa Shinyanga Society Orphanage Centre haihitaji kuwa tegemezi na kwamba wanaweza kulea watoto vizuri endapo serikali itawapatia zana za kufanyia kazi kwa kuwa maeneo ya kuzalisha chakula na mali wanayo bali wanachohitaji ni msaada wa trekta ili kujitegemea.

Vituo vya kulelea watoto yatima vilivyonufaika na msaada huo ni Shinyanga Society Orphanage Centre cha Mjini Shinyanga, Muvuma na Peace Kahama Orphanage Centre vya Mjini Kahama.



Vijana wakivua samaki aina ya kambare katika Mto Kizinga, eneo la Mtoni Mtongani, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kitoweo nyumbani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Abbasi ataka TaSuBa, THT kushirikiana kukuza vipaji

**Na Anitha Jonas**

KATIBU Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbasi, ameielekeza Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSuBa) kuanza kushirikiana na Tanzania House of Talents (THT), katika mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa muziki.

Dk. Abbasi alitoa agizo hilo jana alipotembelea kituo hicho kilichoko jijini Dar es Salaam, kuangalia maendeleo ya vijana wanaolelewa hapo.

THT ilianzishwa na Ruge Mutahaba (sasa marehemu) kwa lengo la kukuza vipaji vya sanaa ya muziki kwa vijana na kuwajengea uwezo wa kujiendeleza.

Akizungumza katika ziara hiyo, Dk. Abbasi, alisema wizara inatambua mchango wa THT katika kukuza tasnia ya muziki na inaheshimu vipaji vya vijana wanaolelewa na taasisi hiyo na pia inafahamu maono ya mwanzilishi wake kuhusu kuendeleza kituo hicho, kwamba iko tayari kuwapa ushirikiano.

"Nitaunganisha wadau wote wenye nia na mapenzi mema ya kukuza sanaa na kuendeleza kituo hiki, nikiwamo mimi mwenyewe ili tuwe walezi wa THT kwa kipindi chote," alisema Dk. Abbasi.

Msimamizi wa Kituo hicho kwa sasa, Kemmy Mutahaba, alisema THT imekuwa ikifanya kazi kwa takribani miaka 15 sasa, lengo kubwa ni kuibua na kukuza vipaji vya vijana katika tasnia ya muziki, ili waweze kujikwamua kiuchumi.

"THT imekuwa ikilea vijana katika misingi ya uzalendo kwa kusimamia msemo huu wa marehemu Ruge kuwa 'Watu wenye njaa ya mafanikio hawatazami ukubwa wa changamoto, wanatazama ukubwa wa ndoto'," alisema Kemmy.

Mama mzazi wa Ruge, Christina Mutahaba, ambaye ndiye mwanzilishi wa kituo hicho, alitoa ombi kwa serikali kuendelea kutoa ushirikiano wa kukiendeleza ili kuishi ndoto za mwanzilishi wake.

Akihitimisha ziara hiyo, Dk. Abbasi alisema serikali itaendelea kushirikiana na kituo hicho.

Katika ziara hiyo, Dk. Abbasi alitembelea studio ya kituo hicho na kuahidi kutafuta wadau watakaosaidia upatikanaji wa vifaa ambavyo ni vibovu.

Pia aliwasihi kushiriki katika Tamasha la Serengeti Music and Arts linaloandaliwa na serikali na linalotarajia kufanyika Desemba 26, mwaka huu.

# St. Mary's kumwenzi Rwakatare kitaaluma

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE za St. Marys zimeahidi kuendelea kufanya vizuri kitaaluma na kusimamia maadili mema kama sehemu ya kumwenzi mwasisi wake, Marehemu Getrude Rwakatare.

Ahadi hiyo ilitolewa juzi mmoja wa wakurugenzi wa shule hizo, Dk. Rose Rwakatare, kwenye mahafali ya shule ya awali Tabata jijini Dar es Salaam.

Alisema watahakikisha taaluma nzuri iliyokuwa ikitolewa na shule hizo wakati wa uhai wa Dk. Rwakatare inaendelea kutolewa kama kawaida.

"Sisi wakurugenzi tulikuwa kwenye shule hizi tangu mwanzilishi akiwa hai, hivyo tutazisimamia vizuri msiwe na wasiwasi hazitatetereke kitaaluma hata kidogo," alisema Dk. Rose Rwakatare.

Pia aliwashukuru wazazi kwa kuendelea kuiamini shule hiyo na kupeleka watoto wao akiahidi kuwa shule zitaendelea kuwalea katika maadili mema kama alivyokuwa akisisitiza mwanzilishi wa shule hizo.

"Hapa watoto wenu wako sehemu sahihi watapata elimu bora siku zote na nyinyi ni mashahidi namna shule hizi zinavyoendelea kufanya vizuri kitaaluma kwa sababu tumejipanga kufanaya makubwa," aliahidi Dk. Rwakatare.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Thomas Balilemwanaye, aliwashukuru wazazi kwa kuendelea kuiamini shule hiyo huku akiwaahidi kuendelea kuwapa elimu bora na kusimamia maadili mema

"Kwa sababu mmetuamini nawaahidi hatutawaangusha tutaendelea kuchapa kazi kuhakikisha shule inaendelea kufanya vizuri kitaaluma na shule hii itaendelea kuwa chaguo sahihi kwa wazazi kwa sababu tuna walimu mahiri sana na mazingira yetu ni mazuri," alisema.

Alisema jambo lingine wanalojivunia ni uongozi mahiri ambao umewawekea mazingira mazuri na kuwafanya kufanya kazi zao kwa ufanisi.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera mawaziri wateule, jamii inasubiri vitendo zaidi

**RAIS** John Magufuli jana alikamilisha uteuzi wa Baraza la Mawaziri likiwa na sura nyingi mpya huku baadhi ya vigogo waliokuwa katika baraza lililopita wakiachwa.

Katika baraza hilo, wamo waliokuwa makatibu wakuu wa wizara ambao wameteuliwa kuwa mawaziri katika wizara nyeti zinazolingana na taaluma zao. Pia Rais ameanzisha wizara mpya ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Mawaziri wapya hao waliokuwa makatibu wakuu ni Dk. Dorothy Gwajima anayekuwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Mhandisi Leonard Chamuriho anayekuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi. Dk. Faustine Ndugulile ameteuliwa kuwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Kabla ya hapo, Dk. Gwajima alikuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais (TAMISEMI) anayeshughulikia Afya wakati Mhandisi Chamuriho alikuwa Katibu Mkuu wa iliyokuwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Pia kuna sura mpya na nafasi zao kwenye mabano kama vile Prof. Kitilla Mkumbo (Ofisi ya Rais Uwekezaji), Geoffrey Mwambe (Viwanda na Biashara), Prof. Adolph Mkenda (Kilimo) na Mashimba Ndaki (Mifugo na Uvuvi). Pia wako waliopanda ambao ni Jumaa Aweso (Maji) na Dk. Damas Ndumbaro (Maliasili na Utalii).

Sambamba na wateule wapya na waliopanda, kuna mawaziri ambao wamerejea kwenye nafasi zao. Mawaziri hao ni William Lukuvi (Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi), Doto Biteko (Madini), Dk. Merdard Kalemani (Nishati), Kapteni mstaafu George Mkuchika (Ofisi ya Rais-Utumishi), George Simbachawene (Mambo ya Ndani ya Nchi), Dk. Mwigulu Nchemba (Katiba na Sheria), Selemani Jafo (Ofisi ya Rais- TAMISEMI) na Jenista Mhagama (Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Uratibu, Bunge, Kazi na Watu wenye Ulemavu).

Licha ya kuwapo kwa mchanganyiko wa mawaziri wa zamani na wapya, katika naibu mawaziri, zimeibuka sura mpya ni za vijana wengi ambao wanaandaliwa kuwa viongozi wa miaka ijayo kama Rais alivyoahidi kuwafikiria vijana zaidi katika serikali yake.

Kwa hali ya kawaida, baraza jipya limeonyesha picha halisi kwamba Rais amedhamiria kuhakikisha anatekeleza yale yote aliyoyaahidi kwenye kampeni za uchaguzi mkuu, mengi yakiwa yameainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Wateule hao, kwa mantiki hiyo, wanapaswa kutambua kwamba Rais amewaamini kuwa wana uwezo katika kutekeleza majukumu yao kupitia wizara watakazoziongoza ili kuleta mageuzi ya kweli ya kiuchumi, hasa kipindi hiki ambacho Tanzania iko katika uchumi wa kati.

Mawaziri hao na manaibu wao, ni lazima pia watambue kuwa kuna kundi la watu wengi ambao walikuwa katika baraza lililopita na sasa wameachwa kwa sababu mbalimbali, hivyo wanapaswa kuchapa kazi na kuleta matokeo ya kweli kulingana na matarajio ya aliyewateua.

Kwa ujumla, kuna matatizo mbalimbali katika kila sekta - iwe ya kiuchumi na kijamii. Mawaziri walioteuliwa pamoja na manaibu wao, wanapaswa kuhakikisha wanatatua kero za wananchi kwani iwapo watashindwa, wataondolewa na nafasi zao kuchukuliwa na wengine.

Tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao, huku wakitanguliza mbele maslahi ya taifa na kutambua kuwa wameingia katika nafasi hizo kwa ajili ya kuwatumikia wananchi na si kujinufaisha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wajasiriamali kumbukeni vifungashio bora siri ya mafanikio katika biashara

**MWONEKANO** wa bidhaa unaweza kumfanya mteja akavutiwa na kununua au asinunue. Hiyo ni kwa sababu mbalimbali ikiwamo vifungashio ambavyo kimsingi ni vya muhimu katika biashara.

Vifungashio vina kazi ya kukinga bidhaa isiharibike, kuvutia na kushawishi, kuwasaidia wateja kufanya uamuzi, na vinasaidia kutofautisha bidhaa sokoni kwa alama ya biashara au muundo uliotumika kuvitengeneza.

Kwa hali hiyo, ni lazima itamvutia mnunuzi, kuamini ubora wa bidhaa iliyomo ndani ya inafanya kazi ya kutoa maelezo ya bidhaa. Hapo ndipo unapokuja umuhimu wa vifungashio.

Hata mafunzo mbalimbali ambayo hutolewa na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TDMA) kuhusu ufungashaji bora wa bidhaa, huonyesha umuhimu kwa kila mfanyabiashara na mjasiriamali kuzingatia vifungashio vya bidhaa zake. Wajasiriamali na wafanyabiashara wanahimizwa kutumia vifungashio vyenye hadhi inayoridhisha kama njia mojawapo ya kutangaza vyema bidhaa zao ili kuvutia wateja waweze kuzinunua.

Kimsingi, ili bidhaa iweze kumvutia mteja, wataalamu wa biashara wanasema, kuna umuhimu wa kuwa tofauti na bidhaa nyingine, kwamba ule upekee wa muundo wa bidhaa ndio huvutia wengi. Mjasiriamali na mfanyabiashara wanatakiwa kuwa na kitu ambacho kitawapa utambulisho wao sokoni. Kwa kuwa kufanya hivyo ni rahisi kwa wateja kutambua bidhaa sokoni kutokana na utofauti wake.

Mfanyabiashara anapokuwa na vifungashio vya aina yake na vyenye ubora, anakuwa katika nafasi nzuri zaidi ya kukabiliana na washindani wake na kumwezesha kupata soko kubwa ama kupata wateja wengi. Huo ndio mwelekeo ambao hata Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara Wenye Viwanda na Kilimo Arusha (TCCIA), Olais Mollel, anahimiza ili wajasiriamali na wafanyabiashara waweze kufanikiwa. Baadhi ya wafanyabiashara na hasa wadogo, wamekuwa na kawaida ya kuvamia biashara bila kuangalia soko linataka nini na mwisho wa siku wanajikuta wamekwama kupiga hatua.

Ili kufanikiwa katika hilo, mkazo zaidi unawekwa katika kuangalia soko kwanza linataka nini ndipo mtu aanzishe biashara, badala ya kuanzisha tu hali ambayo itamfanya ashindwe kupiga hatua.

Aidha, kwenye muundo wa bidhaa, Mollel anataka mfanyabiashara anapotengeneza muundo wa bidhaa asiifikirie kama bidhaa bali afikirie katika muundo wa mtu kwa maana ya yule atakayeinunua. Hivyo vifungashio vya bidhaa vinatakiwa kufikisha ujumbe ama kutoa utambulisho fulani kwa watu wa aina fulani, ili watakapoiona bidhaa iwe rahisi kutambua kuwa bidhaa husika imetengenezwa kwa ajili yao.

Kwa maana hiyo, bidhaa inapoingia sokoni, wateja watachangamkia, hivyo jambo muhimu ni mfanyabiashara kuangalia washindani wake na kujifunza kutoka kwao, ili aweze kutengeneza vifungashio vinavyovutia zaidi.

Vifungashio hivyo vinaweza kusababisha bidhaa kufanya vizuri sokoni, hivyo si vibaya mfanyabiashara kuwekeza fedha nyingi ili kuhakikisha vifungashio ama mwonekano wa bidhaa zake unavutia wateja. Katika kufanikisha hilo, wafanyabiashara wanashauriwa kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya vifungashio bora, ambavyo vitatambulisha vyema bidhaa kwa wateja na hivyo kupata soko la uhakika.

Inaelezwa kuwa si vibaya kila mjasiriamali na mfanyabiashara wakajiweka katika upande wa wateja kwa kujiuliza, kama wao wangekuwa ni wateja wangeweza kununua bidhaa ambayo haijafungwa vizuri?

Hatua ya wao kujiweka kwenye nafasi hiyo, inaweza kuwa njia mojawapo ya kujifunza na kutambua umuhimu wa kutengeneza bidhaa ambazo zitakuwa katika vifungashio vinavyotakiwa.

Kwa sasa wapo baadhi ya watu wanaofanya biashara ya kuuza dagaa wa kukaanga kutoka Mwanza, wapo wanaowafunga katika mifuko ya nailoni, na wengine hutumia vifungashio vyenye mifuniko. Ni imani kwamba yule anayetumia vifungashio vyenye mifuniko, anaweza kupata wateja wengi zaidi kuliko anayeweka ndani ya mifuko ya nailoni na kupeleka sokoni.

Wote wana vifungashio, lakini jambo la msingi ni vile ambavyo ni bora na vinavutia wateja na kujihakikishia kuwa na soko la uhakika na hivyo kuweka kupanua biashara na kuwa kubwa zaidi.

Inawezekana upatikanaji wa vifungashio bora vya bidhaa likawa ni tatizo kwa wafanyabiashara wadogo kutokana na gharama yake, ama kwa sababu nyingine, lakini suala la kuboresha bidhaa ni muhimu.

SAFU

## FIKRA MBADALA



Nkwazi Mhango, Canada

**Watanzania sio wajinga wala wapumbavu kushindwa kupima ushahidi utakaotolewa. Kwa namna ghilba hizi zinavyofanywa, kuna dhana kuwa kuna maadui wa nje ima wanaowatumia wahusika au wahusika kutafuta watu wa kuwatumia ili kufikisha malengo yao.**

# *Mnaichafua Tanzania kupata nini jamani?*

KUMEKUWA na kampeni za makusudi za kupotosha ukweli baada ya kuisha uchaguzi mkuu wa 2020 za kuichafua, kuihujumu na kuisingizia Tanzania. Nasema hivi kutokana na wahusika kutotoa ushahidi wowote unaoingia akilini kutokana na tuhuma zinazoendeshwa na baadhi ya Watanzania.

Mfano hivi karibuni, nilihudhuria mjadala kupitia zoom juu ya mashambulizi ya kigaidi huko Mtwara yaliyofanywa na magaidi toka Msumbiji. Tofauti na mijadala niliyowahi kuhudhuria, huu ulionyesha wazi namna ya waliouandaa walivyolenga kulaumu serikali kwa "kutoshughulikia" kadhia hii jambo ambalo, hadi sasa, sijui kama lina chembe ya ukweli ikizingatiwa kuwa Tanzania haijawahi kuacha kuwalinda wananchi wake. Isitoshe, madai yaliyotolewa ni makubwa mno kuwa magaidi walichoma vijiji na kuua watu ukiachia mbali kuingiza silaha za kivita nchini.

Katika mjadala husika, waandaaji walijigeuza wajuaji na wasemaji wa kila kitu huku wengine tukiachwa. Nilishangaa walivyokuwa wakiteua waulizaji na wajibuji maswali. Yupo mmoja, aliyetoa paka kwenye kapu. Alisema "ni mimi (alitaja jina lake) nataka kuuliza swali." Aliruhusiwa kuongea alivyotaka akitupa madongo yake kwa serikali bila chembe ya ushahidi kiasi cha kutuacha wengi vinywa wazi.

Kuonyesha upande mmoja, hapakuwapo na msemaji wa serikali wala ushahidi kuwa waliitaarifu ikakataa kutoa maelezo au kutuma msemaji wake.

Kwa watu hawa, madaraka hayana maana; wala demokrasia haileti maana bila ya wao kuwa kwenye ulaji. Ama kweli mvunja nchi ni mwananchi! Kama tutakuwa wakweli, Watanzania hata kabla ya kufanya uchaguzi walionyesha kuridhishwa na uongozi wa awamu ya tano ambao kwa kipindi hiki, wamechagua chama tawala kiasi cha kuufuta upinzani, kwa kuazima maneno toka kwa rafiki yangu Mzee Pius Msekwa. Kama nilivyowahi kusema huko nyuma, hii inatokana na serikali kujibu karibu kero zote zilizowasumbua Watanzania tangu kupata uhuru kimsingi, ushindi huu haukusababishwa na kuiba kura au njama yoyote zaidi ya utendaji uliowaridhisha wapigakura. Pamoja na ukweli huu kujulikana, bado wapo wanaoendelea na wimbo ule ule wa kutaka uchaguzi uonekane uliibiwa bila kutoa hata chembe ya ushahidi. Kulalamika ni haki ya wahusika; kudanganya na kuzua si haki. Leteni ushahidi; tuhukumu. Watanzania sio wajinga wala wapumbavu kushindwa kupima ushahidi utakaotolewa. Kwa namna ghilba hizi zinavyofanywa, kuna dhana kuwa kuna maadui wa nje ima wanaowatumia wahusika au wahusika kutafuta watu wa kuwatumia ili kufikisha malengo yao.

Kinachoendelea hata kama kitavikwa kila aina ya sifa za kidemokrasia hakilisaidii taifa wala wale walioko nyuma ya mpango huu ambao mwisho wake ni hasara. Wahusika wangepeleka madai yao kwenye mamlaka husika. Huko nje hakuna msaada wala jibu la tatizo. Madai ya kuibiwa kwa uchaguzi yawe ya msingi au vinginevyo si mapya wala si tatizo kwa Tanzania wala Afrika tu. Hivi karibuni, kwenye uchaguzi uliopita nchi ya Marekani inayojisifia kuwa mwalimu wa demokrasia duniani, yalizuka madai ya kihuni na yasiyo na msingi wala mashiko ambapo rais anayeoondoka alishindwa vibaya. Kwa msingi huo, licha ya kukataa kumpongeza mpinzani wake aliyemshinda kihalali, bado analalamika kuwa aliibiwa ushindi wakati serikali yake ndiyo iliyosimamia uchaguzi husika.

Kwa wanademokrasia wa kweli, kushinda na kushindwa si sababu za kubomoa, kuzushia au kuijengea nchi uhasama kwa kuitangaza vibaya. Kila mtu ana nchi moja aliyopewa na Mungu, yaani alipozaliwa bila kuomba wala kujaza fomu. Wahusika wanaweza kupata uraia nje japo uraia wa karatasi thamani yake ni ndogo ikilinganishwa na ule wa kuzaliwa. Ndiyo maana ukiishi ughaibuni huachi kuonyeshwa kuwa wewe ni wa kuja na huwezi kuwa na haki sawa na wazawa kwa vile wanajua una kwenu. Kwa kuzingatia hili, wanaoichafua, kuizushia na wanaoidhalilisha Tanzania wanafanya hivyo ili kupata nini zaidi ya hasara?

Kitu kinachoshangaza ni ile hali ya wanaotuhumiwa kutoa hata nafasi kwenye kuunda serikali ambayo wahusika walishindwa kuchaguliwa kwenye uchaguzi. Kwa upande wa Zanzibar, umeonyesha mfano wa kuwa kinachogombaniwa si kweli. Kwani, kama wahusika walishindwa na wakakaribishwa kwenye serikali, wanachotafuta cha mno ni nini zaidi ya kuichafua Tanzania bila sababu za msingi?

Tuhitimishe kwa kushauri Watanzania tuwe wazalendo. Tanzania ndiyo nchi yetu pekee. Kwingine hakuna jibu; na kama lipo ni la muda. Wanaoichafua Tanzania wanafanya hivyo kupata nini?

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO



Na Joseph Kulangwa

**Mnyukano huu unafanana na wagonjwa waliokwenda hospitali wakisindikizwa na watu wasiofahamika katika familia zao, na kupokewa na kisha kufikishwa kwa daktari aliyewapima na kuwalaza wodini, na kuendelea kuwahudumia kama wagonjwa wake.**

# *Wabunge CHADEMA wasitutoe macho*

IBARA ya 78(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inasema: "Kwa madhumuni ya uchaguzi wa wabunge wanawake, waliotajwa katika ibara ya 66(1)(b), vyama vya siasa vilivyoshiriki katika uchaguzi mkuu, kwa kufuata utaratibu uliowekwa na kupata angalau asilimia tano ya kura zote halali za wabunge, vitapendekeza kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi majina ya wanawake kwa kuzingatia uwiano wa kura ambazo kila chama kimepata katika uchaguzi wa wabunge."

Ibara hii kwa sasa ndiyo gumzo kwa Watanzania walio wengi wanaojishughulisha na ufuatiliaji wa siasa nchini, zikihusisha uchaguzi wa wabunge wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). Wabunge hawa hujulikana kama wa viti maalumu, ambapo chama hicho kilipata sifa ya kuwa na wabunge hao 19.

Gumzo hilo liliibuka mara tu wabunge hao wakiongozwa na aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake la CHADEMA (BAWACHA), Halima Mdee, kuapishwa Novemba 24 na Spika wa Bunge, Job Ndugai mjini Dodoma, nje ya Bunge.

Suala la kuapishwa nje ya Bunge lilielezwa vizuri na Spika Ndugai, kuwa kuna kanuni zinaruhusu ambazo zilipitishwa na Bunge la 11, ingawa chini chini malalamiko yaliendelea hata kuwekwa wazi na Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, kuwa si sawa, kwani kilichofanyika ni sawa na kuapishwa gereji, huku Ndugai akihimiza kuwa suala ni kuapa mbele ya Spika, kokote kunakofaa.

Hata hivyo, baada ya kiapo hicho na Kamati Kuu ya CHADEMA (CC) kukana kushiriki kuwateua, kwa maana kwamba Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika, hakujua kilichotokea ingawa Mkurugenzi wa NEC, Charles Mahera, aling'ang'ania kukabidhiwa majina hayo na Mnyika, CC ikawavua uanachama wabunge hao.

Lakini wakati ikichukua hatua hiyo kali na ngumu, ikiungwa mkono na BAWACHA na Baraza la Wazee CHADEMA (BAZECHA), bado Ndugai ameshikilia kuwa walioapa ni wabunge halali na wataendelea na shughuli za Bunge ikiwa ni pamoja na kupata stahiki zao za kibunge.

Na baada ya maneno kuongezeka, Mdee akajitokeza kwa niaba ya wenzake, na kusema watakata rufaa Baraza Kuu la CHADEMA kupinga adhabu hiyo na endapo watashindwa, hawatang'ang'ania ubunge, ingawa alisisitiza wataendelea kuwa wanachama wa chama hicho.

Mnyukano huu unafanana na wagonjwa waliokwenda hospitali wakisindikizwa na watu wasiofahamika katika familia zao, na kupokewa na kisha kufikishwa kwa daktari aliyewapima na kuwalaza wodini, na kuendelea kuwahudumia kama wagonjwa wake.

Majumbani, familia hazijui kama ndugu zao wanaumwa na wamefikishwa hospitalini na kulazwa. Daktari hana haja ya kujua wamefikafiaje hapo, kwa kuwa anawaamini wafanyakazi wake wa mapokezi.

Hivyo mwenye siri ya kujua kilichowafikisha wagonjwa hospitalini hapo na hata kumwona daktari, anayebaini wanaumwa kiasi cha kuwalaza, ni mtu au watu wa mapokezi. Wagonjwa ni wabunge hao 19, watu wa mapokezi ni NEC na daktari ni Ndugai. Hivyo kwa gumzo linaloendelea, Daktari Ndugai hana makosa kabisa na hana haja ya kubishana na ndugu wa wagonjwa, kwani anaona wana sifa ya kulazwa (kuingia bungeni), halikadhalika familia hazina sababu ya kumtolea macho, kwani ana huruma ya kidaktari.

NEC ndiyo inapaswa kujibu iliwapokeaje wabunge hao, nani alikabidhi majina hayo na hatimaye kuapishwa, huku uongozi wa CHADEMA ukiwa hauna habari, kwani Katiba inautaka uteue majina na kuyapeleka NEC. NEC haina mamlaka ya kuorodhesha majina na kuyapeleka bungeni kuapishwa.

Kama ni kweli majina hayo yalitoka kwa Katibu Mkuu wa CHADEMA tena baada ya kikao cha CC, je, NEC ilishindwa nini kuthibitisha kabla ya kuyapeleka bungeni? Hakuna kinachoshindikana, kama ilivyotokea Novemba 30 kwenye mechi ya Ligi Kuu ya Soka Bara katika uwanja wa Kumbukumbu ya Karume, Musoma, ambapo lilitokea kosa likarekebishwa na mambo yakaendelea.

Ilikuwa mechi kati ya Biashara United Mara na Azam FC ambapo mwamuzi kimakosa alipuliza kipenga cha kumaliza mchezo katika dakika ya 89 badala ya 90, lakini alipobaini saa imempoteza, akabadili uamuzi na mechi ikaendelea mpaka kukamilika. Hakuna lililoharibika. Hili la CHADEMA lina ugumu gani? Alamsiki!

## KONA YA UKWELI

# Viongozi waliopewa dhamana watatue kero za wananchi



Na Thobias Mwanakatwe

BAADA ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu Oktoba 28, mwaka huu, hatimaye wamepatikana madiwani, wabunge na wawakilishi ambao moja ya majukumu yao ni kuwatumikia wananchi waliowachagua kwa kuwa wao ndio kiunganishi kati ya wananchi na serikali.

Miongoni mwa hoja zinazotolewa pindi zinapotokea kasoro katika utendaji ni kujipima kama mhusika anafaa kuendelea kuwa kwenye nafasi anayoitumikia kwa wakati huo na unaweza kuwa na msukumo kutoka kwa mtu au kikundi cha watu kulinganana na mahitaji na kubwa zaidi msukumo unaweza kutoka kwa mwajiri.

Katika kujipima na kuachia mamlaka ili kutoa nafasi kwa wengine wanaoona kuwa wanafaa huwa mara nyingi ni kipimo cha kiongozi aliye makini na baadaye wanajamii wanaweza kumkumbuka kwa ujasiri wa kuikabili hali hiyo.

Katika mazingira ya aina hiyo, ni dhahiri kuwa kila mmoja na hasa wenye ofisi za umma au zozote zenye kutoa huduma kwa umma, wanapopewa ushauri au mwaliko wa kujipima, hicho ndicho huwa kipimo kuwa wanajali kwa kiasi gani maslahi ya wananchi walio wengi dhidi ya maslahi binafsi.

Kiongozi anapopata fursa ya uongozi anatakiwa kufanya hivyo kwa niaba ya wananchi walio wengi; na ili aongoze vyema kuna mkataba unaomwelekeza.

Mwanafalsafa Jean-Jacques Rousseau (1712-1778) katikac kazi yake ya "The Social Contract (1762) aliwahi kusema kiongozi anafanya yale anayoelekezwa na wananchi na si anayotaka yeye.

Kwa mtazamo rahisi tu, ni viongozi wangapi hivi leo wanazingatia kauli ya mwanafalsafa huyo? Wengi wamekuwa hawafuati makubaliano baina yao na wananchi na kwa hali hiyo, wanalazimika kuacha mamlaka kwa wananchi wengine ili waongoze.

Hali hiyo inajibainisha kwa kuzingatia kauli ya mwanafalsafa wa Kiingereza, John Locke (1632-1704) ambaye alisema kiongozi mzuri anatakiwa awe na kumbukumbu ya makubaliano yake na wananchi moyoni mwake, vinginevyo aachie mamlaka au kwa maneno mengine aachie ngazi.

Kwa kiwango kikubwa, viongozi wanatakiwa kujiangalia kwenye kioo kuhakiki kiwango cha uzalendo walio nao. Hapo ndipo panapotakiwa kujiangalia kama wanafaa kwenye nafasi zao za utumishi au la.

Jambo linalogomba hapo ni dhana ya utumishi maslahi badala ya utumishi wa umma kwa kufuata maelekezo ya mikataba baina yao na wananchi.

Katika nchi ambayo inaamini kwenye mfumo wa demokrasia utendaji unaoonyesha kwenda kinyume cha mahitaji yanayofungamanishwa na demokrasia ambayo ni uhuru kwa mwananchi kushiriki moja kwa moja katika kujadili na kutoa maamuzi kwa mambo yote yanayoihusu jamii na yeye mwenyewe unakuwa ni utendaji batili. Hali hiyo inamaanisha kuwa, kila mtu angependa kushiriki yeye binafsi, lakini kwa kuwa idadi ya watu ni kubwa mno na hivyo kuwa ni vigumu kuwakutanisha wote kwa pamoja, kwa sababu si rahisi kuweka watu wote kwa pamoja sehemu moja kujadili yanayowahusu.

Kwa kuzingatia hali hiyo, ndani ya mfumo wa kidemokrasia ndio unakuwapo uwakilishi kupitia Bunge ambao unamaanisha kuwa walio wengi wanawachagua wachache ambao wanawaamini kuwa wana akili timamu na uwezo kama sio ujuzi ili kuwawakilisha kwenye kuyafanyia maamuzi na kupata ufumbuzi wa matakwa na mahitaji yao.

Kimsingi, kupitia mfumo huu haimaanishi kuwa utendaji wa kidemokrasia unaweza kufanyika kiholela bali ni namna ya ushiriki hubadilika au utendaji hubadilika kwa kuwapa fursa wananchi kutoa nafasi ya ajira kwa wawakilishi kupitia chaguzi ambazo mara nyingi huhesabika kuwa ni huru na za haki pia. Chaguzi hizo ni huru na za haki kwa maana hazina uchakachuaji.

Katika ajira hiyo wanatakiwa kulinda na kuwezesha majadiliano yaliyo huru na yenye ukweli ndani yake na katika mazingira ambayo hayatatofautiana na uwepo wa watu wale wanaowawakilisha kwa kuzingatia kuwa kama nafasi hiyo ingewezekana kupatikana na wangekuwapo ndani ya kumbi za bunge.

Katika mazingira hayo mbunge au mwakilishi ambaye anaingia ndani ya bunge na kwenda kinyume na ajira aliyopewa na wananchi, huyo wakati akijinadi kuomba ajira hiyo alikuwa na yake moyoni kuwa alikuwa anaomba kula si kura. Hawa wa aina hii ni wengi na ndio wanaokiuka mikataba baina yao na wananchi. Hawa ndio wachumia tumbo.

Majadiliano huru, haki na ukweli Bungeni, vina lengo la kuikosoa serikali ili iwatumikie vyema wananchi walioiweka madarakani. Lakini inapotokea majadiliano kutokuwa kwenye mizania inayokubalika hilo huifanya mioyo ya waliowapa ajira kunyong'onyea na kujikuta wakikata tamaa na kujishika tamaa kwamba walitoa ajira kwa wasiowajibika kwao.

Ili kujiondoa kwenye maudhi kwa waajiri (wananchi) ni kutumia uhuru na demokrasia iliyopo kukubali yanayokidhi matakwa ya waajiri na kuyakataa yale yanayowaudhi wanaowawakilisha.

Kimsingi ni kwamba ajira ya uwakilishi inatokana kwa wananchi hivyo uwakilishi unapaswa kuongozwa na matakwa ya wanaowakilishwa badala ya kuongozwa na ushabiki usio na tija. Ni muhimu kujenga fikra sahihi kwamba watoa ajira wanatakiwa kuheshimiwa pamoja na matakwa yao chanya kwani wao wanabakia wakiwa kimya wakiwa na subira yenye heri lakini mambo yanapokwenda kinyume huwataacha kuikumbuka kauli ya Martin Luther King aliyowahi kusema: "Maisha yetu huanza kuonekana hayana maana pale tunapokuwa kimya wakati mambo yasiyofaa yanaendelea kufanyika mbele yetu."

**● Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com**

## DARASA LA NDOA

# Mambo muhimu ya kuzingatia na kuyaepuka katika uchumba



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka 0744000066

JUMAPILI iliyopita tulijadili kwa kina mambo ya kuzingatia kuanzia urafiki kwenda uchumba ikiwa ni mchakato wa kuelekea kwenye ndoa. Katika mwendelezo wa safu hii, leo tutaangazia uchumba na mambo yanayopaswa kuzingatiwa.

Kwanza kabisa, uchumba ni daraja la kuingia katika ndoa na mchumba huwa ni mmoja tu. Uchumba una msimu na hautakiwi kuwa wa muda mrefu. Uchumba unatakiwa hudumu katika kipindi cha mwaka mmoja na usizidi miaka miwili kabla ya ndoa.

Yako mambo ya kujifunza zaidi katika kipindi cha uchumba. Watu wanaweza kutumia muda mrefu wa kujifunza na kufahamiana wakiwa katika urafiki, lakini si katika uchumba.

Kinachotokea kabla ya ndoa, ndicho kitakachotokea wakati wa ndoa. Mchumba wako akiwa na hasira wakati wa uchumba, basi ujue akiwa katika ndoa atakuwa zaidi. Mchumba akiwa mwongo au akiwa na tamaa, basi baada ya ndoa atakuwa balaa.

Pamoja kuwa mapenzi ni upofu, ni muhimu kuchukua tahadhari pale viashiria vibaya vinapojitokeza wakati wa uchumba. Usilazimishe uchumba kama huna hakika na mchumba wako.

Waswahili wanasema "Heri ya nusu shari kuliko shari kamili." Ukiolewa na mtu asiye sahihi, baada ya ndoa utavuna maumivu. Uchumba si ndoa bali ni hatua ya msingi ya ndoa. Hivyo, uchumba huweza kuvunjika.

Makosa yakifanyika katika uchumba, yanaathiri ndoa. Kwa hiyo, ni muhimu kufanya maamuzi makini katika uchumba. Mfahamu vizuri unayemchumbia, kwani waswahili wanasema "si vyote ving'aavyo ni dhahabu."

MAMBO YA KUZINGATIA

Yako mambo kadhaa ya kuzingatia katika kipindi cha uchumba. Kwanza kabisa, uwe na kusudi maishani. Usifurahie na kuvutiwa na sherehe za ndoa za wengine, bali jiulize kwa nini unataka kuoa au kuolewa? Umejipangaje kuwa mume au mke wa mtu? Si watu wote wana sifa za kuwa waume au wake za watu.

Pili, pata muda wa kutosha wa kumfahamu mtu. Chunguza na jiridhishe ikiwa ni pamoja na mila na desturi. Pima upendo wake kama niwa bandia. Upendo wa kweli hauvutwi na mali, fedha, vitu au mwonekano pekee.

Sura, cheo, elimu, umbo/sura visiwe vigezo pekee katika kumchagua mtu. Nenda mbali zaidi. Fahamu haiba yake.

Tatu, mshirikishie Mungu kikamilifu. Kupata mwenzi anayefaa ni mtihani mzito. Usitumainie akili zako. Huwezi kupata mwenzi anayefaa Mungu asipohusika. Mwenzi mwema hutoka kwa Mungu.

Nne, epuka uamuzi wenye mashinikizo. Kuoa au kuolewa ni hiari. Usioe au kuolewa kwa mashinikizo. Uamuzi makini unahitajika kwani uamuzi wa siku moja unaweza kujenga au kubomoa maisha yako yote.

Tano, zingatia muda. Tambua wakati mwafaka wa kufanya uamuzi wa ndiyo au hapana kwani hata katika hatua ya uchumba kuna nafasi ya kufanya maamuzi thabiti.

Muda wa uchumba ni muda wa kupokea majibu ya Mungu kwamba ndiyo au hapana. Tambua tabia hatarishi mapema.

Sita, pima uwezo wake wa kufikiri, kushauri na kuamua mambo. Maisha ni kusaidiana na kushauriana. Haifai kuwa tegemezi kwa kila kitu hata kwa mawazo. Pima uwezo wa mchumba wako katika kufikiri, kushauri na kufanya maamuzi.

Saba, epuka uchumba wa siri. Washirikishe wazazi, walezi na ndugu zako. Ndoa si jambo la siri, hivyo kuchagua mwenzi ni wajibu binafsi, lakini ni vyema kushirikisha wazazi/walezi kwa ushauri zaidi.

Vijana wengi siku hizi hawashirikishi wazazi au walezi wao mchakato wa kumpata mwenzi, bali hushirikisha uamuzi ambao wameyafanya tayari. Hali hii imesababisha wazazi au walezi wengi kuwa watekelezaji wa uamuzi wa watoto wao badala ya kuwa washiriki au washauri. Hali hii imesababisha matatizo katika ndoa za vijana wengi.

Nane,tengenezeni muda wa kukutana na kuzungumza mambo ya msingi. Kuzungumza ana kwa ana kunasaidia kufahamiana zaidi. Huo ni wakati kushirikishana hisia kila mmoja alizo nazo na pia ni wakati wa kuandaa mpango mkakati wa ndoa. Huu pia wakati wa kuwekana wazi kuhusu matarajio katika ndoa.

Tisa, pimeni afya. Ni muhimu kujiridhisha kuhusu ukamilifu wa afya ya mwili na akili. Hii itasaidia kama kuna matatizo yafahamike na kushughulikiwa mapema.

Kumi, ni wakati wa kujifunza zaidi kuhusu masuala ya ndoa. Nyumba hujengwa kwa hekima, ufahamu na maarifa. Bidii ya kujifunza mambo yanayohusu taasisi ya ndoa ni muhimu sana.

Wachumba wawe na kiu ya kufahamu misingi, kanuni, na taratibu za ndoa, kwani wakisha oana maisha hayatakuwa kama walivyozoea. Mfumo wa maisha unabadilika. Hivyo, wawe tayari kuyakabili mabadiliko.

UTAJUAJE KUWA NDIYE?

Jambo la kutambua kuwa uliyemchagua ndiye sahihi lina umuhimu mkubwa sana katika maisha ya uchumba hadi ndoa. Ni muhimu kwa sababu anachukua sehemu kubwa ya moyo na mawazo yako.

Pia utamtambua kwa sababu unajisikia amani na furaha moyoni. Ngono, mali, fedha au vitu siyo kipaumbele chake. Anakupenda jinsi ulivyo, anatamani sana uwepo wako na anapenda mawasiliano ya mara kwa mara.

Utamjua pia akiwa anaonyesha moyo wa kujali, anaonyesha hali ya kuwa mvumilivu na subira, si king'ang'anizi wala mtu wa haraka na papara na anaonyesha uwezo wa kuchukuliana na hali yako. Sambamba na hilo, anakuheshimu na kujiheshimu, na anakubalika na wazazi au walezi wako.

Mwisho kabisa, vijana hawana budi kujiepusha na uhusiano hatarishi usio na tija katika maisha yao.

**● Dk. Mlyuka ni Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare) asasi inayojihusisha na masuala ya ndoa na malezi ya watoto. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa baruapepe: info@tamcare.or.tz**

# MAISHA

Desemba 6, 2020
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



HARUSI

Ukurasa 12





**Namna ya kuandaa soseji ya mboga**

Ukurasa 14

Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Jinsi ya kusafisha sofa lenye kitambaa



‘BULL RING’

# Pete ya pua inayompamba mwanamke

Ukurasa 14

# Ukali huchangia madhara kwa wasichana

**Na Moses Ismail**

WAKATI alipokuwa anarudi nyumbani, akitokea tuisheni, mkaka mmoja wa mtaani alimwita mahali pasipokuwa na watu. Aliogopa kwenda, lakini yule mkaka akamshika kwa nguvu na kusogea naye kichochoroni na kuanza kumshika 'sehemu mbaya'.

Kitendo hicho alikitarajia. Wenzake wengi mtaani wameshamsimulia habari za kushikwa shikwa na kaka huyo, huku akiwatishiwa kuwa wakisema kwa watu atawaua. Wengine pia ameshawahi kuwafanyia mchezo mbaya.

Bahati yake ni kuwa wakati alipokuwa naye kichochoroni, kwa mbali walitokea watu wazima na kusababisha huyo kaka amuache aende zake kwa ahadi kuwa kesho akitoka tuisheni wakutane mahali hapa na asipotokea, siku nyingine akimkamata atamuua.

Hilo linalomsumbua. Anaogopa kuuliwa na anaogopa pia kufanyiwa 'mchezo mbaya' na huyo mkaka ambaye wenzake wanamsifia kuwa anavuta bangi na anaweza kumchoma mtu yeyote kisu bila ya kukamatwa.

Lakini anawezaje kufungua 'domo lake' na kukueleza maswahibu hayo yaliyomkuta leo? Anaogopa. Kinachomwogopesha ni jinsi wewe mzazi wake utakavyolipokea jambo hilo na kumgeuzia yeye mwenyewe kibao na kumwangushia kichapo.

Ndio, anajua hilo litatokea. Anajua kuwa utamuuliza ilikuwaje akachelewa tuisheni kiasi hicho mpaka akakutana na huyo mkaka? Anajua lazima utahisi hayo ndio mambo anayofanya siku zote na ungemchapa tu. Historia ya malezi yako haimpi ujasiri wa kukuambia. Anabaki amenyamaza akiugulia moyoni.

Siku ya pili anapoenda tuisheni, jambo hilo bado linamsumbua akilini na najua siku hiyo ndio siku ya kukutana na yule mkaka. Anaamua kumsimulia mtoto mwenzake anayesoma naye juu ya suala hilo na mtoto huyo naye anamweleza mwalimu wa tuisheni na mwalimu naye analifanyia kazi kwa kuripoti polisi.

Ukiwa nyumbani, saa moja usiku, huku ukiapia kwa miungu yako jinsi utakavyomwadhibu kwa kuchelewa kurudi nyumbani mpaka saa hizo, unastuka kuona polisi wamefika nyumbani kwako na mwalimu wa tuisheni na kukusimulia namna walivyoweka mtego wa kumponya mwanao asibakwe. Unaduaa!

Haraka unamshika na kumkubatia kwa hisia mchanganyiko wa hofu na shukurani. Anashnagaa na kuangusha chozi huku akihofia mwalimu na polisi wakiondoka tu lazima umchape. Lakini leo humchapi, badala yake unaongea naye vizuri na unamuuliza kwa nini hakukuambia mapema? Hakujibu, ananyaza kimya.

Akijibu nini? Kuwa aliogopa utamchapa kama siku ile alivyokuambia kina John wanamchezo wa kumchungulia na ukamwambia yeye ndiye anayefanya wamchungulie? Au akuambie umchape kama ulivyomchapa kwa mambo mengine mengi alivyofanyiwa na kuamini ana haki ya kukuambia?

Huu ni mfano tu wa sababu za watoto wengi wanaobakwa, wengine kwa muda mrefu. Kwamba ukali wa wazazi wao wenyewe ndio chanzo cha kupatwa na mikasa hiyo kwa kutowapa watoto hao nafasi ya kuwaeleza yale yaliyowatokea kwa sababu ya ukali wao unaowanyima nafasi ya kuongea kirafiki.

## QUIZ

NA HAMIS KIDAGO
0657 207168

### LE QUIZ DU WEEK

1. Nyumbua kitenzi "Être" kama maelezo yanavyoonesha hapo chini.

Conditionnel
Présent
Je ..................
Tu ..................
Il/elle ..................
Nous ..................
Vous ..................
Ils/ells ..................

Passé
J' ..............................
Tu ..............................
Il/elle ..............................
Nous ..............................
Vous ..............................
Ils/elles ..............................

2. Nyumbua kitenzi "Être" katika "Infinitif" présent na passé.
- Présent
- Passé..............

3. Weka kitenzi "Être" katika Participe présent na passé.

- Présent.........
- Passé............
..................

4. Pangilia kitenzi "Être" katika Impératif présent na passé.
- Présent......
.............
.............
- Passé............
..................
..................

### MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA

Le quiz du week – end
- Nyumbua kitenzi "Être" kama maelezo yanavyoonesha hapo chini.


Conditionnel
Présent
Je serais
Tu serais
Il/elle serait
Nous serions
Vous seriez
Ils/ells seraient

Passé
J' aurais été
Tu aurais été
Il/elle aurait été
Nous aurions été
Vous auriez été
Ils/elles auraient été


- Nyumbua kitenzi "Être" katika "Infinitif" présent na passé.
  - =Présent être
  - = Passé avoir été
- Weka kitenzi "Être" katika Participe présent na passé.
  - =Présent étant
  - = Passé été
  ayant été
- Pangilia kitenzi "Être" katika Impératif présent na passé.
  - =Présent sois
  soyons
  soyez
  - = Passé aie été
  ayons été
  ayez été

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA KIDOGO



Konokono analeta athari zipi kwa binadamu?

**Mazungumzo kati ya marafiki wawili yalikuwa kama ifuatavyo;**
**Juma: Habari yako kijana?**
**John: Safi tu niambie,**
**Juma: Aiseee! Muda kweli naona unaangaika na bodaboda tatizo nini kwani?**
**John: Dah! Namsaidia huyu kijana Raymond kutafuta kiki za haraka aonekane kwenye gazeti eti.**
**Juma: Ooohhhh!! Kweli huyu mzima!**

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Usiangalie na kutafakari tatizo bali tafuta chanzo

KARIBU tena msomaji katika safu yetu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Nimepokea ujumbe mbalimbali toka kwa wasomaji wetu kuhusu yanayowasibu. Wengi inaonekana hawajui chanzo cha matatizo yao pasipo kufunuliwa, kwani vyanzo vipo ila hawavitambui.

Nitajaribu kutaja baadhi ya vyanzo kwa kuvitolea mifano kwa wale yaliyowakuta na kwanini wanataabika leo.

Watu wengi tunaangalia na kutafakari tatizo, hatutaki kujua chanzo chake ni nini.

Ni mara nyingi tumejifunza kwamba matatizo mengi yanaanzia katika ulimwengu wa roho (ule ulimwengu usioonekana kwa macho ya kibinadamu). Na pengine wengine wamezaliwa na hayo matatizo kwa kuambukizwa toka tumboni mwa mama zao. Lakini wengine wameyakuta matatizo utotoni.

Hata hivyo chanzo kikubwa cha matatizo yote ni nguvu za giza. Yawezekana na uchawi, mapepo, mizimu, roho za kurithi. Lakini katika matatizo yote haya, kila tatizo lina roho nyuma yake.

Yupo mama mmoja alikuwa na pepo la udhaifu. Alikuwa amepinda mgongo kwa miaka 18. Haikuwa udhaifu kama udhaifu, bali ndani yake kulikuwa na pepo la udhaifu.

Mwingine akawa na pepo bubu, haongei. Mwanadamu ataona ni kawaida tu, kumbe nyuma yake kuna roho. Walipoombewa walipona.

Tuangalie mafarakano kwenye ndoa nyingi. Moja ya vyanzo ni pepo linalosababisha. Zipo roho ambazo ni za tangu kizazi na kizazi. Usiangalie tu kwamba ni mafarakano, tafuta chanzo.

Matatizo mengine chanzo chake ni dhambi. Unapoishi maisha ya dhambi, unafungulia mlango wa matatizo.

Ni kweli watu wanaombewa, lakini mbona tatizo linarudi? Maisha yako unaishije? Dhambi ni mlango unaoruhusu mateso uliyo nayo.

Vipo vyanzo vingi vya matatizo. Unaweza ukayasababisha wewe mwenyewe. Au matatizo ukasababishiwa na vizazi vilivyopita. Lakini yaweza kuletwa na watu wako wa karibu waliokuzunguka.

Baba zetu, mababu na mabibi walitenda dhambi, walishakufa lakini sisi tumechukua maovu yao. Kwa maneno mengine tunachukua adhabu ya dhambi waliyotenda.

Adhabu inatujia sisi kwa sababu ni dhambi ambayo haikutubiwa. Hakuna hata mmoja aliyetubu kwa ajili ya ile dhambi iliyotendwa na vizazi vilivyopita. Au tusema kwamba tunakula matunda ya mti dhambi.

Pamoja na hayo, husukumwa na chanzo (mzizi). Ili ulishughulikie tatizo liishe, chunguza mzizi wake. Na ili uukate mti usiweze kumea tena ni lazima uchimbue mzizi, maana mzizi ndio chanzo cha kuendelea kumea mti.

Mpenzi msomaji, kama babu zetu walitenda dhambi, walimwaga damu, waliua, lakini hakuna mtu aliyewahi kutubu uovu au dhambi hiyo, iwe unajua au hujui pengine aliua hakumweleza mtu yoyote, lakini ile damu ilimwagika, inaweza kuendelea kudai kizazi hadi kizazi.

Hiyo ni kwa sababu hakuna aliyewahi kutubu juu ya dhambi hiyo. Unapotenda dhambi leo, unapanda mti na yale matunda unaweza usiyale, wala usipokee adhabu wewe, wakapokea adhabu watoto wako au wajukuu zako.

Ndio maana hata Mungu anasema katika maandiko yake kwamba “Nami nawabatiliza (anawalipiza) wana wa maovu yao tangu kizazi cha kwanza kilichotenda dhambi mpaka kizazi cha nne.”

Ipo misukosuko mingi ya kimaisha inayowapata watu, huku wengine wakidhani wamerogwa kumbe katika kizazi chao, yapo mambo yaliyofanyika pasipo wao kujua yanaweza kuleta athari katika maisha yao.

Kwenye koo kama za machifu/watemi yalifanyika maagano mengi ambayo yalifanywa na watu ambao leo hawapo duniani. Maagano kwa mfano ya kufanya matambiko kila mwaka. Mengine yaliwekwa kutoa kafara binadamu wenzao.

Ndio maana katika baadhi ya familia utasikia kila ikifika mwezi au tarehe fulani kila mwaka lazima mmoja wa wanafamilia afe.

Anaweza kuugua ghafla au akapatwa na ajali mbaya ili mradi tu damu inamwagika kutimiza agano lililowekwa na mababu ambao leo hawapo. Hizi ni athari zinazotokana na chanzo.

Mpenzi msomaji wangu, leo naishia hapa. Wiki ijayo nitaeleza vyanzo zaidi vinavyofanya watu wataabike leo iwe ni kwenye ndoa, afya au uchumi. Je, unayo maoni, ushauri au kisa tujadili kwa pamoja? Nitumie 0715268581. Namba hii pia ipo WhatsAPP

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Jamii ishiriki kikamilifu kupinga ukatili wa kujinsia

DESEMBA 10 ni kilele cha maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia ambazo zilianza Novemba 25, huku kila anayeshuka kwa namna mbalimbali akifanya jambo kuonyesha kuungano mkono suala.

Katika siku hizo kuna kuwa na visa mkasa vya wanawake waliofanyiwa ukatili na jinsi waliweza kujikwamua na kusonga mbele kimaisha, pasipo kuziangalia changamoto, jambo ambalo litakuwa ushuhuda kwa wengine kuonyesha kuwa inawezekana.

Katika maadhimisho haya, changamoto mbalimbali ziliibuliwa ikiwamo kushamiri kwa wanaotendewa matukio ya kikatili kumaliza kesi nyumbani katika kupingana na mkono wa sheria.

Miaka ya nyuma, kilio kikubwa kilikuwa kukosekana kwa sheria ambazo zinatoa adhabu kali kwa wanaotenda matukio ya ukatili dhidi ya wengine.

Sasa sheria zipo baadhi ya watu wanashirikiana na waliowatendea ukatili kuzuia mkono wa sheria.

Iwapo watafanikiwa kufikishwa mbele ya mkono wa sheria, baadhi huharibu ushahidi au kutokutoa kabisa, jambo ambalo husababisha kesi kushindwa kuendelea na ikiendelea kwa ushahidi uliotolewa haiwi na mwisho mzuri.

Mifano inayotolewa ni kama tukio la mama aliyekatwa mkono na mumewe kwa sababu ya wivu wa mapenzi.

Alishtaki polisi na watetezi wa haki za binadamu wakaanza kufuatilia kwa karibu, lakini baadaye wawili hao walielewana na mtetezi alivyofuatilia aliambiwa ni kiherehere chake.

Kama haitoshi, tukio lingine ni mke kusukumwa ghorofani na kuvunjika taya na nyonga, lakini baadaye alisamehe na kuamua kutoendelea na kesi pasipo kumjulisha mtetezi wa haki za binadamu aliyekuwa anafuatilia kwa karibu.

Lingine lililoibuliwa ni watetezi wa haki za binadamu wa kiume kusingiziwa kuwa na mahusiano na walalamikaji hasa inapotokea aliyetendewa ubaya ni mwanamke na kesi iko kwa mtetezi mwanamume, jambo ambalo linawavunja moyo kuwatetea wengine.

Malalamiko haya yako pia kwa mamlaka zinazosimamia sheria kama polisi na zinazotafsri sheria kama Mahakama zimejikuta katika wakati mgumu kwa kuwa wanaofungua kesi hawarudi au hawatoi ushirikiano licha ya tukio kuwa kubwa.

Mathalani, mtoto alibakwa au kunajisiwa na mwanafamilia, vikao vya kifamilia vinafanyika, wanalipa faini za kimila ni kumaliza kesi huku mila na desturi zilitumika kuendeleza maumivu kama baadhi kutumia majani maalum yanayoheshimiwa kimila kuomba msamaha au kutumia wazee wa kimila.

Kwa mfano kwa kabila la Wachaga jani linaloheshimiwa na hutumika kuombea msamaha ni Isale na kimila mtu yeyote aliyekukosea anapokuja na jani hilo mbele yako moja kwa moja unapaswa kumsamehe.

Unapopeleka kesi mahakamani unakuwa umekwenda kinyume cha utaratibu au makubaliano ya kimila na jamii inayokuzunguka itakushangaa kukutenga.

Wengi wamejikuta katika mazingira magumu kimaamuzi kwa kuwa anaogopa kutengwa na jamii yake inamlazimu kuondoke kesi mahakamani au polisi ili wamalizane nyumbani, na iwapo watalazimishwa kuendelea basi huharibu ushahidi.

Kinachosahaulika ni maumivu ya kisaikolojia aliyoyapata aliyetendewa ubaya huo, na aliyekwenda kuona kuna mwanya wa yeye kuomba msamaha na mambo yakaisha kienyeji bila mkono wa sheria wa kwenda jela miaka 30 au zaidi kumwondoka, jamba ambalo halifai na halikubaliki katika kuisimamia jamii.

Kwa sasa kutokana na kukua kwa miundo ya upashanaji habari na taarifa, matukio yanapotokea husambaa kirahisi na kuripotiwa na vyombo vya habari kila mahali.

Kutokana na hali hiyo, kuna ongezeko la matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto ambayo yanaripotiwa na vyombo mbalimbali na kwenye mitandao ya kijamii.

Ni wajibu wa jamii kutoyafumbia macho matukio haya, ni lazima mkono wa sheria uwepo ili kutoa haki kwa wote, ili kukomesha vitendo hivyo kwamba anayetaka kutenda kabla ya kufanya hivyo akumbuke kuna kifungo cha miaka 30 jela au zaidi.

Ushirikiano wa jamii ni muhimu sana ili kuondoa uwezekano wa kuharibu kesi, kwa kuwa zipo kesi zimekwama kutokana na mashahidi kutotoa ushahidi au mbinu ovu kutumika kuharibu ushahidi.

Tunapokuwa na jamii yenye watoto waliobakwa maana yake wameathirika kisaikolojia na hali hiyo huwafanya kutojiamini na kujiona nao ni sehemu ya jamii na inawapenda.

Kama ni mtoto wa kiume aliyenajisiwa maana yake ameharibiwa hataweza kuwa baba wa baadaye jambo ambalo halitakiwa kwa kuwa tunaua kizazi cha baadaye, tunakuza kizazi kisicho na maadili ya kiafrika na zaidi ni kumkosea Mungu na kufuru kubwa sana.

**Tutafakari!**
**Mungu ibariki Tanzania.**





# Henry & Bahati

Henry Mbilinyi na Bahati Hoza, ndio wanaotupambia ukurasa wetu leo. Ndoa ilifungwa Kanisa la Kiinjili la Kilutheli Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Iringa, Novemba 22, 2020.







# MITINDO







# 'WEEKEND' PENSI YA JEANS ITAKUFAA ZAIDI

KUNA wakati unataka kuvaa nguo nyepesi ambazo zitakupa furaha hasa siku za mwishoni mwa wiki. Kwa mfano unataka kwenda matembezini au kukutana na ndugu, jamaa au marafiki ukiwa na mwonekano tofauti, lakini wenye mvuto zaidi.

Huna sababu ya kukata tamaa kwa kuhofia kutazamwa vibaya, kwani kuna aina ya mavazi yatakufanya upendeze.

Vazi la kaptula ya Jeans, inatosha kukupatia furaha na mtazamo mpya unapoamua kuvinjari maeneo mbalimbali.

Kaptula ya Jeans ambayo mitaani wanaita 'Pensi' ni suluhisho tosha baada ya kuchoshwa na suruali au nguo zingine ambazo unaitumia muda mwingi wakati wa shughuli za kikazi.

**JINSI YA KUCHAGUA**

Tafuta kaptula ambayo ina ukubwa unaolingana na mwili wako, hakikisha inabana kiasi ili kukuweka katika mtazamo mzuri.

Wengi wanapenda iliyoshonwa katika mtindo wa kisasa 'Model' ambayo inabana kuanzia kiunoni hadi mapajani.

KITAMBAA

Hakikisha nguo yako inatokana na kitambaa cha pamba halisi. Kama mchanganyiko basi tafuta ile ya pamba yenye asilimia 90 na malighafi nyingine asilimia 10.

Hii inatokana na vitambaa vingi si halisi na inaweza kukupa usumbufu wa kuongezeka kwa ukubwa pale unapofua.

**RANGI**

Angalia rangi isiyong'aa sana kwa lengo la kukupa uhuru wa kuvaa na nguo yoyote ile. Jeans yenye rangi mpauko ni nzuri zaidi kwani inamtoa mtu yoyote.

**PIGILIA JUU**

Unaweza kuvaa kaptula ya Jeans na nguo za aina mbalimbali kama fulana, shati na jacketi.



## UREMBO

# 'BULL RING' Pete ya pua inayompamba mwanamke

UVAAJI wa pete ya ringi maarufu kama 'Bull Ring' umeanza kupata umaarufu miongoni mwa wanawake katika nchi za Afrika Mashariki.

Mapambo ya aina hii yanatumika kwa kiasi kikubwa katika nchi ya India, lakini kutokana na kupendwa na idadi kubwa ya watu, matumizi yake yanaendelea kusambaa duniani kote.

Wataalamu wa masuala ya urembo, wanasema uvaaji wa 'Bull Ring' upo kwa jinsi zote, lakini wanawake ndio wanaoongoza hasa kutokana na kupenda kujiremba zaidi.

UVAAJI WAKE

Kuna aina mbili ya uvaaji wa vipini vya 'Bull Ring', wapo wanaopenda kutoboa chini ya pua na kuna wale wanaopenda kuvaa ya kubandika.

Wanaopenda kuvaa ya kutoboa, ni lazima kuhakikisha wanakuwa wasafi muda wote hasa kwa kuzingatia pini inatengenezwa kwa chuma, shaba au madini ya dhahabu.

Kwa ujumla, mlimbwende anaweza kuvaa aina yoyote ya p ambo hili akaonekana na mvuto wa kipekee.

## MAPISHI
### Na Mary Geofrey

# NAMNA YA KUANDAA SOSEJI YA MBOGA

SALADI ni chakula chepesi, kinakupa nguvu za kutosha na kuzuia adha zinazotokana na kushiba kupita kiasi.

Chakula hiki kina nyama kiasi ambayo inaweza kukupa nguvu zaidi, hasa kwa wale wanaopenda kula nyama katika kila mlo.

**Mahitaji**

Kabichi, nyanya, vitunguu, spinach, pilipili hoho, Mafuta ya Oliva, Limao au vinegar au ndimu, chumvi kiasi na Soseji

**Namna ya kuandaa**

Anza kuandaa soseji kwa kuzichemsha na maji, weka chumvi kiasi na acha ziive.

Kata mboga za majani kwenye vipande vidogo na weka kwenye sahani.

Kata nyanya, pilipili hoho, karoti kwenye vipande vidogo, kisha changanya na salad yako.

Kata soseji kwenye vipande vidogo na changanya kwenye salad

Changanya vinegar, limao au ndimu na mafuta ya Olive pembeni kwenye bakuli kisha koroga vizuri hadi ziwe sawia.

Nyunyuzia mchanganyiko wa limao au ndimu au vinegar na oil juu ya salad. Nyunyuzia kuzunguka salad, usirundike sehemu moja.

Weka chumvi kiasi kisha anza kuchanganya

Kumbuka, salad inaliwa ikiwa ya baridi, hauna haja ya kupasha moto.



# MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

## JINSI YA KUSAFISHA SOFA LENYE KITAMBAA



WASWAHILI husema 'umaridadi huficha umaskini' hii ni sentesi nzuri kwa kutamkwa, lakini inatafakarisha.

Katika kona ya nyumba, leo nataka tuangalie umaridadi katika usafi wa sofa kwa sababu hili nalo ni kiungo muhimu cha kung`arisha na kuleta mvuto ndani ya nyumba.

Na hili nalo kama ilivyo katika mambo mengine kwenye nyumba, linahitaji usafi tena kwa umaridadi wa hali ya juu hususani kwa nyumba zenye familia kubwa.

Baadhi huwa hatuna utaratibu wa kusafisha sofa zetu mara kwa mara pengine kwa kutokujua vitu vinavyotumika kusafishia na mahali pa kuvipata.

Sofa zikifutwa kawaida au kwa kutumia maji matokeo yake huwa sio mazuri kwa kuwa badala ya kung`ara huanza kuchafuka na kuchakaa zaidi.

Kwa wale wanaomiliki sofa za vitambaa, wanatakiwa kutumia njia sahihi zaidi ya kusafisha badala ya kufuta kienyeji ili kuzitunza zisiharibike kwa sababu kitambaa kiko katika hatari zaidi ya kuharibika endapo utaratibu mzuri hautafuatwa wakati wa kusafisha.

Yapo maji maalum au kwa lugha ya kigeni 'spray' inayotumika kusafishia sofa hizo, ni vyema ukaitafuta hiyo kwa sababu inapatikana kwa wingi madukani.

Lakini kabla ya kuanza kutumia, hakikisha sofa zako zimepanguswa na kutolewa vumbi iliyokuwa imeng`ang`ania kwa kutumia kifaa maalum cha kupuliza vumbi ama kwa kutumia kitambaa kisafi.

Baada ya kusafisha kila kona, unatakiwa kuanza kupulizia spray.

Kwa kuzingatia ujazo katika chupa hizo maalum za maji ya kusafishia sofa, unaweza kutambua utumie chupa ngapi na kwa sofa ngapi hasa kulingana na ukubwa wa tatizo japokuwa naamini moja inaweza kutosha labda kama imechafuka kupitiliza.

Unachopaswa kufanya ni kupulizia kidogo kidogo kwenye sehemu zilizochafuka na wakati huo huo uwe unafuta na kitambaa kisafi mpaka umalize.

Baada ya kumaliza kazi hiyo unaweza kuliacha likauke na hapo ndipo utaanza kuona matokeo mazuri, kwa sababu mng`ao wa rangi yake utakuwa mzuri zaidi.

Kumbuka kwamba kufanya usafi huo katika sofa lako hauhitaji gharama kubwa sana endapo utafanya mwenyewe, isipokuwa uamue kutumia gharama kubwa kwa matakwa yako kwa kutumia wataalamu wa kukodi.

Pia, kadri utakavyojenga utaratibu wa kupenda kusafisha sofa lako mara kwa mara ndivyo hivyo gharama itazidi kuwa ndogo kwa sababu hutatumia spray nyingi kama ambavyo utasafisha zikiwa zimechafuka sana.

# MPANGILIO

## DONDOO MUHIMU ZA KUFANYA FENICHA ZAKO ZIWE NA MATUMIZI ZAIDI YA MOJA



1: Meza ya kuwekea vipodozi inaweza iwe na hitaji zaidi ya moja kama droo za kuhifadhia vitu mbalimbali.
2: Kitanda kiwe na droo za uvunguni ambazo unaweza kuhifadhia shuka, taulo na mablanketi ya ziada.
3: Kabati la nguo, unaweza kuweka droo za kuwekea nyaraka zako muhimu pamoja na kioo cha kujitazamia.
4: Flemu za picha ukutani ziwe na uwezo wa kuondoa na kuweka picha muda wowote.

# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO... ...MABAYA YAKE LAKINI MEMA ANAYO.

# Waliokufa miaka 2,000 wapatikana

**ROMA, Italia**

WANASAYANSI wa mambo ya kale wagundua mabaki ya wanaume wawili waliofariki dunia katika mlipuko wa volkano ulioharibu mji wa kale wa Roma wa Pompeii, karibu miaka 2,000 iliyopita.

Wataalamu hao walisema maiti hizo zilikuwa za mwanaume ambaye alikuwa wa hadhi ya juu na mwingine alikuwa na dalili ya kuwa mtumwa.

Mkurugenzi wa eneo hilo, Massimo Ossana, alisema yawezekana watu hao walikuwa wanatafuta hifadhi baada ya kutokea mlipuko huo ambao uliangamiza maelfu ya watu.

Mji wa Pompeii ulikumbwa na mlipuko wa volkano kutoka Mlima Vesuvius, katika mwaka AD 79.

Mlipuko huo ulifunika mji wa Pompeii kwa jivu la moto na kusitisha shughuli za mji huo na wakazi wake.

Kwa sasa mji huo umekuwa chanzo muhimu cha wanakiolojia katika utafiti.

Maofisa hao walisema mwanaume huyo tajiri alikuwa na umri katika 30 na 40, ambaye alipatikana akiwa na nguo ya kifahari ya kujikinga baridi chini ya shingo yake.

Mwanaume mwingine ambaye alisemekana kuwa kati ya umri wa miaka 18 na 23, mfupa wake uliokuwa umevunjika katika mwili na kuashiria alikuwa mtumwa aliyefanya kazi za mkono. Miili yao iligeuka kuwa kama matabaka na kuonyesha kuwa ilikuwa imeingia kwenye jivu hilo la volkano.

**BBC**



Wanaume wawili wa Kipalestina wakimbeba mtoto wa simba kwa ajili ya kuwaonyesha watoto wanaoishi katika kambi ya wakimbizi ya Rafah, kaskazini mwa ukanda wa Gaza jana. **(PICHA: REUTERS)**

# Iran yakataa masharti mapya ya Marekani

**TEHRAN, Iran**

IRAN imesema haitakubali masharti mapya aliyoyatoa Rais mteule wa Marekani, Joe Biden, kuhusu kufufua makubaliano ya mpango wa kinyuklia wa nchi hiyo.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, Javad Zarif, alisema Marekani inatakiwa kurudi katika meza ya makubaliano ya mwaka 2015 kabla ya kufanyika mazungumzo mapya.

Biden hivi karibuni alisema atairudisha nchi yake katika meza ya majadiliano ya mkataba wa kinyuklia na kuondoa vikwazo, kama Iran itakapofuata makubaliano ya mkataba huo. Kila upande inaonekana kutaka upande mwengine kufuata masharti ya makubaliano hayo kwanza.

Mwaka 2018, Rais wa Marekani, Donald Trump, alijiondoa katika mkataba huo ambao ulifanikiwa katika utawala wa Barrack Obama.

Baadaye aliiwekea vikwazo vikali vya kiuchumi vikilenga biashara ya mafuta na sekta za kifedha. Hata hivyo, Iran imepitisha viwango vya mpango wake wa kinyuklia na kuibua wasiwasi huenda itatengeneza bomu la kinyuklia.

Akihutubia mkutano kupitia mtandao ulioandaliwa na Itali Alhamisi, Zarrif alisema Marekani imekuwa ikikiuka makubaliano ya Umoja wa Mataifa wa kuondoka katika makubaliano hayo.

"Marekani ni sharti kukoma kukiuka sheria za Umoja wa Mataifa," alisema.

Alisema hatua hiyo inahitaji majadiliano na kwamba taifa hilo halina nafasi ya kuweka masharti mapya.

**BBC**

# Urusi kuanza kutoa chanjo Covid-19

**MOSCOW, Urusi**

JOPO la wataalamu wa afya nchini Urusi, limeanza kusambaza chanjo ya virusi vya corona inayoitwa Sputnik V, katika kliniki 70 zitakazotoa huduma hiyo.

Tukio hilo litakuwa la kwanza kubwa la utoaji chanjo ya Covid-19 kufanywa nchini humo.

"Raia walio kwenye kundi lililo katika hatari ambao katika kazi zao wanakutana na waathirika wengi wa virusi hivyo, wanaweza kupewa chanjo hiyo," walisema maofisa wa jopo hilo.

Jana maofisa wa afya katika mji wa Moscow, walisema watakaopewa chanjo hiyo katika awamu ya kwanza ni watu wasiozidi umri wa miaka 60, huku watu wenye magonjwa mengine, wanawake wajawazito na wanaonyonyesha watoto hawatapewa chanjo.

Meya wa Moscow, Sergei Sobyanin, aliandika katika tovuti yake binafsi kuwa watu wengi wamejisajili kupatiwa chanjo hiyo.

"Katika saa tano zilizopita watu 5,000 wamejisajili kwa chanjo hiyo, walimu, madaktari, wafanyakazi wa jamii na wale ambao leo hii wanayahatarisha maisha yao zaidi."

Utoaji wa chanjo hiyo umeanza, wakati nchi hiyo imeweka rekodi ya maambukizi ya watu 28,782 kwa siku moja. Idadi hiyo imefikisha watu 2,431, 731 wamepata virusi hivyo tangu kuanza kwa janga hilo la virusi vya corona. Licha ya ongezeko la maambukizi, Urusi haijaweka vikwazo vyovyote kwa raia wake kama inavyofanya nchi zingine za Ulaya.

Mwezi uliopita Wizara ya Ulinzi ya Urusi, ilitangaza kuendesha operesheni kubwa ya utoaji chanjo kwa wanajeshi 400,000 na mwishoni mwa mwaka huu.

**DW**

# Marekani kuwaondoa wanajeshi wake Somalia

**WASHINGTON, Marekani**

HATUA ya Rais wa Marekani, Donald Trump, kuwaondoa wanajeshi wa Marekani nchini Somalia, katika muda wake wa mwisho imewashangaza wengi.

Seneta Ayub Ismail Yusuf, mwanachama wa kamati ya masuala ya mambo ya kigeni nchini Marekani, alisema katika taarifa yake kuwa uamuzi wa Trump wa kuondoa wanajeshi hao, wakati muhimu katika mapambano dhidi ya wanamgambo wa Al Shabaab pamoja na mtandao wao wa kigaidi ni kitendo cha kujutia.

Yusuf alisema wanajeshi wa Marekani wamechangia kiasi kikubwa kwa jeshi la Somalia kwa kutoa mafunzo na ushauri.

Hata hivyo, serikali ya Somalia bado haijatoa tamko lolote kuhusu uamuzi huo uliotolewa juzi, ambao utawahusiha wanajeshi 700 watakaoanza kuondoka kuanzia Januari 15 mwakani.

**Dw**

MAKALA

# Kujitolea kunalipa - 2



Na Magabilo Masambu

**Unapokuwa tayari kufanya kazi za kujitolea kwa bidii na maarifa katika maeneo mbalimbali, utakutana na watu wa kada tofauti na wenye uzoefu. Ingawa ni kweli hupati kipato unachokihitaji kwa wakati huo, lakini bado unakuwa na fursa ya kujitengenezea mtandao muhimu wa watu wanaoweza kukufaa katika safari yako ya kutafuta ajira.**

SEHEMU hii ni mwendelezo wa makala iliyopita juu ya umuhimu wa kujitolea. Kwa kifupi nilieleza namna mhitimu anavyoweza kujitolea kufanya kazi ya kitaaluma, badala ya kusubiri kuajiriwa au kupita ofisi moja hadi nyingine kwa ajili ya kutafuta kazi.

Mhitimu wa chuo cha ualimu kwa mfano, wakati akisubiri ajira ya ualimu, anaweza kuomba kujitolea kufundisha katika shule ya kata iliyoko kijijini kwake. Faida kubwa atakuwa ameongeza kundi la Watanzania watakaomfahamu, maana wanafunzi huwa hawabaki kuwa wanafunzi siku zote, bali huweza kuwa watu wenye nyadhifa kubwa zaidi, huko mbeleni. Kwa hiyo kwa kuwafundisha tayari utakuwa umejitengenezea pia hazina ya baadaye, japo lengo la kujitolea halipaswi kulenga kujiwekea hazina ila ikiwapo hatuachi kuitumia.

Pia hii inahusisha kuhamasisha wengine katika shughuli za maendeleo. Unapojitolea unawafanya watu wengine wakuone kama mfano na kuigwa na washiriki katika shughuli mbalimbali za jamii, ili kujiletea maendeleo. Haitakuwa lazima kusubiri viongozi wa eneo husika, kutatua matatizo yao.

Kama unaweza kufanya kazi za bure, maana yake ni kwamba kazi zako binafsi utazifanya vizuri zaidi, litakuwa jambo la ajabu sana kama unaweza kufanya kazi za watu wengine kwa kujitolea na kazi zako za kimaendeleo zikushinde, badala yake tunaamini kwamba utazifanya kwa usitadi mkubwa zaidi maana zinahusu zaidi maisha yako.

Kujiongezea mtandao wa kiajira. Katika siku za leo, mtandao wa ajira ni hitaji muhimu. Mtu anayefahamiana na watu wengi kwenye maeneo mbalimbali ya kikazi, anajiongezea fursa ya kuunganishwa na taarifa za kiajira. Siku hizi wanasema watu ni mtaji.

Aina ya mitandao ya kiajira tunayoijenga, mara nyingi hutegemea tunafahamiana na watu wa aina gani. Kwa hiyo si kazi nyepesi, kwa mfano, kijana anayetoka kwenye familia za tabaka la chini kijijini, kufahamiana na watu wengi mjini wanaoweza kumpa taarifa za kiajira anazozihitaji. Ili kupata taarifa hizo muhimu, kijana huyu hujikuta akitumia nguvu nyingi sana zisizolingana na matokeo.

Unapokuwa tayari kufanya kazi za kujitolea kwa bidii na maarifa katika maeneo mbalimbali, utakutana na watu wa kada tofauti na wenye uzoefu. Ingawa ni kweli hupati kipato unachokihitaji kwa wakati huo, lakini bado unakuwa na fursa ya kujitengenezea mtandao muhimu wa watu wanaoweza kukufaa katika safari yako ya kutafuta ajira.

**UHALIFU**

Hili linawahusu hasa wanaomaliza ngazi mbalimbali za elimu, ambao wengi wao hukaa sana mitaani wakisubiri kuajiriwa. Kama huna kazi ya kufanya ni bora ukajitolea kwa sababu, kuna msemo wa kiswahili unasema "Mtembea bure si sawa na mkaa bure", ukitembea bure unaweza kuokota chochote kuliko ukikaa bure.

Ukijenga mazoea ya kujitolea, unakuwa umetumia muda wako vizuri, muda ambao ungeweza kuutumia kutenda maovu kama ulevi, wizi, ukabaji na mengineyo unautumia katika kujitolea mahali fulani.

Baadhi ya wahitimu wanaona ni sawa kujiingiza kwenye uovu, kwa kuikomoa serikali ama taasisi zisizotoa ajira, kwa kusema ngoja nivute au nilewe tu maana ajira zenyewe siku hizi hakuna. Unachopaswa kufahamu hapa haumkomoi yeyote zaidi yako na familia yako, hata masuala ya ugaidi pia yanatajwa kuwa na vijana wengi ambao wanaingia huko kwa kigezo cha kutokuwa na ajira, lakini inamaana gani hasa kujitafutia ajira ambazo, utazifanya kwa kuweka rehani maisha na familia yako?

Changamoto katika kujitolea hazikosekani. Moja ni kukatishwa tamaa na watu wa karibu. Hii ni kwa sababu jamii kwa sasa inao mtazamo kuwa, fedha ndio kila kitu na kwamba huwezi kufanya jambo lolote bila malipo, hili huwakatisha tamaa wale wote wenye nia ya kusaidia jamii.

Kwa upande wa waajiri katka kampuni binafsi au ya umma. Waajiri wengi hutumia nafasi hiyo pia kuwakandamiza wanaojitolea kwa kuwatumia muda mrefu katika uzalishaji, bila kuheshimu muda wao wa kujitolea.

Baadhi ya waajiri huacha kabisa kuajiri ili kuwatumia wanaojitolea na hivyo watu wengi huona kama wananyonywa, kukandamizwa na kufanywa watumwa, hivyo kuwavunja moyo wenye nia ya kujitolea. Ni kweli kwamba si kazi za malipo, lakini kwa mtu mwenye busara unafanya ubinadamu kidogo kanauli, kachai na hata kalanchi! Isiwe sasa ndiyo umepata watumwa haifai.

Kujitolea si kwa wasio na ajira au kazi za kufanya tu bali ni kwa kila mtu kwani upo ukweli wa kitafiti kwamba unapowafanya wengine wawe na furaha, unakuwa na furaha zaidi.

Tuache hulka za kibepari kwamba, kila unalolifanya lazima likuingizie fedha, fedha hazijai na hakuna siku zitatosha mpaka umauti unatukuta. Hatuwezi kubadilisha mambo mengi kwa fedha bali kwa kujitoa na kusaidia katika wakati ambao tunakuwa na muda wa ziada au hata kutenga kutoka katika muda wetu tulionao katika kazi zetu za jumla.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Unazikumbuka Mzizima United, Mazengo Warriors Taif Cup?



Na Adam Fungamwango

**Na kweli mchezaji mwenye kipaji atasalia Dar tu. Taifa Cup mara nyingi ilikuwa ikichezwa kwenye Uwanja wa Karume, awali ukijulikana kama Ilala Stadium. Wachezaji bora wote kutoka pambe zote za Tanzania walikuwa wanakusanyika sehemu moja kuonyeshana soka linavyosakatwa.**

MNAKAA kwenye redio, mtangazaji anasema "Sasa tunawapeleka kwenye Uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam kusikiliza maelezo ya mpira wa miguu, michuano ya Kombe la Taifa (Taifa). Leo ni kati ya timu ya mkoa wa Dar es Salaam 'Mzizima United' na timu ya mkoa wa Dodoma, 'Mazengo Warriors'.

Hiyo ilikuwa miaka ya nyuma, wakati hiyo michuano ya Kombe la Taifa, ikiwa juu. Ilikuwa michuano maarufu zaidi nchini Tanzania ukiondoa Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara ambayo ndiyo Ligi Kuu ya sasa.

Hii ndiyo michuano mikongwe zaidi. Ni michuano ambayo ilikuwa inazishirikisha timu za mikoa. Mikoa yote Tanzania Bara ilikuwa ikiunda timu za soka na kushiriki michuano hiyo ambayo ilijizolea mashabiki wengi.

Taifa Cup, ni michuano ambayo ilitoa wachezaji wengi ambao walikuja kuzichezea klabu kubwa za Simba na Yanga. Klabu hizo zilikuwa zikiifanya michuano hiyo kama kioo chao cha kutafuta wachezaji wa kuwasajili.

Na kweli ilikuwa michuano iliyokuwa ikikusanya vipaji vingi kutoka kila kona ya nchi na kuiweka sehemu moja, ikawa ni rahisi tu kwa klabu zinazotaka wachezaji kuwachukua.

Uzuri wa michuano hii ilikuwa inaleta wachezaji kutoka ndani kabisa vijijini na kuwapeleka mjini ili kuonyesha vipaji vyao. Mchezaji ambaye ana kipaji alikuwa akifika Dar, harejei tena mkoani. Anasajiliwa na klabu za Dar, kazi imekwisha.

Mfano kama ni mkoa wa Tabora unatafuta kikosi cha mkoa huo. Viongozi wa chama cha soka wanazunguka mijini na vijijini kusaka vipaji au wanaanzisha mashindano kwa klabu mbalimbali za mijini na vijijini. Wachezaji walioonyesha uwezo na wenye vipaji, walichukuliwa kutengeneza timu ya mkoa huo na baadaye wakati kwenda kucheza Taifa Cup, timu inachujwa na inayobaki inapelekwa kwenye michuano.

Ndiyo maana michuano hiyo ilikuwa inawawezesha hata wachezaji kutoka vijijini kuonekana. Wengine unaweza kukuta walikuwa hawajawahi kuishi hata Tabora mjini, lakini anatapa nafasi ya kutoka labda Usoke na kwenda moja kwa moja Dar es Salaam ambako mara nyingi ndiyo ilikuwa ikifanyikia michuano hiyo.

Na kweli mchezaji mwenye kipaji atasalia Dar tu. Taifa Cup mara nyingi ilikuwa ikichezwa kwenye Uwanja wa Karume, awali ukijulikana kama Ilala Stadium. Wachezaji bora wote kutoka pambe zote za Tanzania walikuwa wanakusanyika sehemu moja kuonyeshana soka linavyosakatwa.

Hata hivyo, historia ya michuano hiyo inasema Dar es Salaam ndiyo imechukua kombe hilo mara nyingi zaidi, ikiwa imetwaa mara 12, tangu mwaka 1964 hadi ilipokoma mwaka 2011.

Ukiangalia sababu kubwa si tu kuwa michuano hiyo mara zote inachezwa Dar tu ila kila mwaka inapochezwa michuano hiyo, baadhi ya wachezaji wanabaki Dar kwa kusajili na Simba, Yanga na tuu zingine, kwa hiyo mwaka unaofuata wanakuwa wana sifa za kuichezea timu ya mkoa wa Dar na si mikoa waliotoka tena. Ni kwa sababu moja ya kanuni ya michuano hiyo ni kwamba mchezaji anatakiwa achezee mkoa anaoishi au klabu inayochezea.

Ni wachezaji wengi sana ambao michuano hiyo iliwatoa na kuonekana na klabu za Simba na Yanga ambao ukiwaandika hapa majina yao hawatoshi.

Wachezaji walionufaika zaidi ni kutoka Morogoro, Tanga, Kigoma na Mwanza kidogo. Hiyo ndiyo mikoa iliyokuwa ikizalisha vipaji vingi na kuilisha Dar es Salaam ambayo ikawa inawatumia kwenye michuano hiyo wanapohamia Dar.

Kwa miaka ya karibuni michuano hiyo ikaanza kukosa nguvu, baada ya kanuni nyingi kuongezwa, Dar ikagawanyika ikawa zikawa timu tatu za Ilala, Temeke na Kinondoni.

Lakini ikatengenezwa kanuni kuwa kila mkoa uchezeshe wachezaji watano tu wa Ligi Kuu. Hii ni baada ya mikoa mingi kuacha kuzalisha wachezaji wengi wenye vipaji.

Michuano hii iliyoanza mwaka 1964, ilivutia mashabiki wengi waliokuwa wakijazana Ilala, wengine wakisikiliza kwenye redio. Kila mwaka Dar ilikuwa ikipata shida licha ya kubakisha mastaa, lakini mwakani, timu za mikoa zinakuja na wachezaji wengine wazuri kuliko wale. Lakini nao wanabaki tena.

Burudani nyingine ilikuwa ni majina ya timu hizo za mikoa, ambapo timu ya mkoa wa Dar es Salaam ilijulikana kama Mzizima United, Arusha ilijulikana kama Meru Warriors, Dodoma yenyewe ilikuwa inaitwa Mazengo Warriors.

Timu ya mkoa wa Iringa yenyewe ilijulikana kama Ruaha Star na ile ya mkoa wa Lindi ilifahamika kwa jina la Ilulu Stars na majirani zao timu ya mkoa wa Mtwara iliitwa Mabibo Stars.

Ile ya mkoa wa Kigoma iliitwa Kigoma Stars na timu ya mkoa wa Kagera ilijulikana kama Lweru Eagles, ya Mbeya iliitwa Mapinduzi Stars na Mwanza yenyewe ni Mwanza Heroes.

Tabora ilijulikana kama Mashujaa wa Unyanyembe na Shinyanga ni Igembe Nsabo. Morogoro iliitwa Moro Stars na Tanga iliitwa hivyo hivyo Tanga Stars.

# HADITHI

WASWAHILI wanasema mshika mawili moja humponyoka na karamu mbili zilimshinda fisi. Cecilia, msichana mwenye kila sifa ya kuitwa msichana mrembo, anaangukia kwenye mapenzi ya vijana wawili. Mmoja ni fukara na mwingine mwenye uwezo. Kutokana na mwenyewe Cecilia kutokuwa na msimamo wenye kueleweka, anawaingiza vijana hao kwenye chuki na visasi, vilivyoambatana na wivu uliopindukia na kusababisha maafa makubwa. Ni kisa cha kusikitisha, kutisha na kuhuzunisha, lakini chenye elimu kubwa.

# Adui Namba Moja – 11

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

ZAHIR alimhadithia hatua moja mpaka nyingine aliyotumia hadi kumwondoa duniani Mashaka.

Jasho lilimtoka Cecy, nusura azimie. Alijiona ni kama yeye ndiye aliyemuua Mashaka. Hasira zilizidi kumpanda. Ni kama alipandisha mashetani hivi. Alimsukuma Zahir kwa nguvu akaangukia kitandani.

Hakuwa na nguvu yoyote kutokana na kuzidiwa zaidi na pombe. Kila dakika zilivyozidi kusonga mbele ndiyo ilionekana analewa zaidi kiasi cha kutaka kutokwa na fahamu.

Cecy akauendea mkoba wake. Akaufungua. Akachukua kitu ambacho alitaka kuchukua. Akaufunga mkoba. Akamwangalia Zahir kwa namna polisi anavyomwangalia jambazi. Zahir hakung'amua hilo.

Aliondoa baadhi ya nguo zake na kumwendea kimahaba. Kutokana na ulevi, Zahir hakuona kitu ambacho alishika Cecy mkononi.

Badala yake alimuona mwanamke huyo alimwangukia kitandani na kuhisi kugusana na ngozi nyororo, ilioanza kumpapasa na kumfariji.

Na kweli alifarijika. Ghafla alihisi kitu kama sindano hivi ikimchoma kwenye mbavu. Awali maumivu hayakuwa makubwa sana. Baadaye alihisi maumivi makali ambayo hayavumiliki.


Aliamua kuona nguvu zimuisha. Hakujua nini kimetokea. Alitaka kupiga kelele. Lakini mkono na Cecy ulitua kwenye mdomo wake na kuziba.

Pombe na maumivu makali yalisababisha nguvu zizidi kupungua na kutoweza kabisa kuutoa mkono wake.

Alihisi kitu kingine kikipenya kwenye kifuani na kumfanya ajihisi kama anapaa. Halafu anaanguka kwenye shimo lisilokuwa na kina.

"Mpumbavu mkubwa wee. Yaani umuue mpenzi wangu mimi nikuache. Mashaka mpenzi wangu nimelipa. Nimekulipia. Niliacha siku nakuzika kuwa yeyote atakayekuwa amekuua sitomuacha salama." Alisema huku akikusanya alichotaka kukusanya. Hakuna aliyemwona akiondoka ikiwa ni majira ya saa 3:00 usiku. Kila mtu kwenye hoteli hiyo alikuwa ameshachangamka kwa kilevi.

*************************




**Nimeamua kuchukua uamuzi huu mgumu kwa sababu ambazo nitazitaja. Mimi nilikutana siku moja kwenye daladala na kijana mmoja aliyeitwa Mashaka. Hakuwa na kipato kikubwa, lakini alikuwa na upendo.**

Naomba baba na mama yangu wanisamehe. Naomba familia yangu yote inisamehe. Naomba walimwengu wote mnisamehe.

Nimeamua kuchukua uamuzi huu mgumu kwa sababu ambazo nitazitaja. Mimi nilikutana siku moja kwenye daladala na kijana mmoja aliyeitwa Mashaka. Hakuwa na kipato kikubwa, lakini alikuwa na upendo.

Alinijali, alinipenda. Alinidekeza, nikadeka mtoto wa kike. Nilijiona mtu katika watu. Mwanamke utake nini kama unajua kuna mtu anakupenda na kukujali. Mashaka ni mwanamume anayejua kupenda. Anayejua thamani na mtu, mpenzi na binadamu mwenzake.

Mashaka si tu kwamba nilikuwa mpenzi wake. Nilikuwa rafiki yake pia. Alikuwa mcheshi kwangu. Tukikutana wakati mwingine tunakuwa kama watoto wadogo. Tutataniana. Tutapeana hadithi za uongo na kweli na kuchekesha. Vibonzo, kiasi kwamba ilitufanya kuwa kama kitu kimoja.

Tulizoeana kiasi kwamba hakuna aliyemhofia mwenzake kwa chochote kile.

Lakini mmoja akipata shida, tunageuka kuwa washauri. Tunashauriana. Hata kama hana pesa, anaweza kukushauri kwa mawazo. Mashaka unaweza ukawa na shida ya pesa akakwambia hana. Lakini siyo kama hatokupa. Anaweza kukaa wiki bila kukwambia, halafu akakwita na kukupa bila wewe kutarajia.

Mashaka hakunipenda mimi tu. Kwa sababu alinipenda, alihakikisha kila ninachokipenda mimi anakithamini. Nia yake ni kuwa alitaka niwe na furaha, faraja na amani. Alipenda familia yangu, ndugu zangu na hata kitu chochote anachoona mimi nakipenda.

Tukiwa wapenzi tunakuwa wapenzi kweli. Tukiwa marafiki tunakuwa marafiki kweli. Tukianza utundu kama watoto wadogo, tunakuwa hivyo hadi utashangaa. Maisha yangu na Mashaka yalikuwa hivyo. Tayari nilijiwekea kuwa ndiyo atakuwa nguzo ya maisha yangu.

Kwa bahati mbaya sana akatokea kijana mwingine anaitwa Zahir. Hapa ndipo ninapojutia uamuzi wangu kwenye maisha. Alinilaghai nikalaghaika. Mimi ni binadamu. Nina udhaifu. Kwa kutumia pesa zake, akanibadilisha akili. Nikaanza kumchukua Mashaka hadi kumwacha na kuwa na mapenzi na Zahir. Nilidhani wanaume wote ndivyo walivyo, kumbe sivyo. Alivyo Mashaka sivyo alivyo Zahir.

Pamoja na kwamba ana pesa, hana upendo. Mimi nilihadaika na pesa zake. Pesa nilipata, lakini sikupata upendo. Nilizoea kupetiwapetiwa. Kudekezwa na Mashaka. Kitu hicho sikukipata kwa Zahir. Nikaona hata pesa zake zote kwangu ni bure. Kama mwanamume kuna kitu nilikuwa nimekosa. Nikaona ni bora nirudi kwa Mashaka ili nirudi kuwa mwanamke na si chombo cha kutumiwa.

Zahir alinihitaji tu pale aliponihitaji. Hana kauli nzuri. Habembelezi, ana kiburi na maneno ya kashfa, dharau, kejeli na masimango. Nilivumilia, lakini nikashindwa. Nikarudi kwa Mashaka.

Ni kama nilikuwa nimefuga joka ambalo limenitafuna mwenyewe. Zahir hakutaka tena nirudi kwa Mashaka. Mapenzi yangu na Mashaka kwa mara ya pili yalikuwa ya kuwindwa. Hatukuwa na furaha tena. Zahir akalipiza kisasi. Akamuua Mashaka bila sababu yoyote. Hili ndilo pigo kubwa kwenye maisha yangu.

Kumuua Mashaka ni sawa na kuniua mimi. Lengo la Zahir ni kwamba amuue Mashaka ili nibaki na yeye.

Adui yake namba moja alikuwa ni Mashaka. Aliona akifa basi pingamizi hakuna. Hakufikiri sawasawa. Bora angeniua mimi angemwacha Mashaka wangu. Hakuwa na kosa lolote. Mimi ndiye mwenye makosa.

Nasikitika sana, Mashaka amekufa kwa ajili yangu. Taa yangu ya maisha imepotea. Nani atanipenda hapa duniani kama Mashaka? Nani atanijali? Nani ananidekeza. Nani atajali hisia zangu? Watakaosema wananipenda ni wengi. Lakini hawatakuwa kama Mashaka.

Kwa sababu hiyo mimi nikaamua kuchukua jukumu zito. Jukumu ambalo sikufikiria katika maisha yangu kama nitakuja kulifanya.

Haiwezekani mtu aliyeniulia Mashaka wangu aendelee kuvuta pumzi ya dunia, wakati Mashaka ametulia tuli kaburini. Aendelee kula bata duniani, huku aliyemdhulumu nafsi yake akiwa futi sita chini ya ardhi. Nimeamua kumlipia kisasi. Mimi ndiye niliyemuua Zahir.

Ulikuwa waraka mrefu ulioandikwa na Cecilia. Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni aliuonyesha mbele ya waandishi wa habari. Hii ni baada ya mtu mmoja aliyejulikana kwa jina la Zahir kuuawa kwenye hoteli ya Coconut jijini Dar es Salaam.

"Uchunguzi wetu unaonyesha kuwa kijana aliyeuawa kwenye hoteli hiyo, ameuawa na msichana aliyejulikana kama Cecilia, ambaye waraka huu tumeukuta nyumbani kwao Kinondoni." Alisema Kamanda.

**INAENDELEA JUMAPILI**

HABARI BURUDANI



## FEROOZ ATAMANI WAKATI URUDI NYUMA

MSANII mkongwe wa muziki wa kizazi kipya, Ferooz, amesema wimbo wake wa 'Starehe' ambao ulipata umaarufu nchini, alipanga kuimba na rapa wawili pekee ambao wana vipaji vya hali ya juu.

Wimbo huo ulimpatia zawadi ya gari kutoka kwa Rais wa awamu ya tatu Hayati Benjamin William Mkapa, ambaye aliupenda kutokana na ujumbe wake.

"Wimbo wangu wa Starehe 'idea' niliitoa kwa Rais wa awamu ya tatu marehemu Benjamin William Mkapa, alitusihi wasanii kutunga nyimbo za kuelimisha watu kuhusu Ukimwi".

"Kila nilipokuwa natafuta mtu ambaye nataka asimame kama daktari akili inaishia kwa Prof. Jay, kama ningemkosa basi Mwana Fa alitakiwa asimame, hata Prof. Jay naye hakujua kama nilikuwa nimejipanga hivyo".

Aidha, ameongeza kusema "Napenda apatikane msanii mwingine ambaye atafanya nyimbo ambayo itaishi kama wimbo wa Starehe ambao umedumu kwa muda mrefu."



# ABDU KIBA APATA KIGUGUMIZI

MWANAMUZIKI kutoka Kings Music Records, Abdu Kiba, amejikuta akipata kigugumizi kusema ukweli kile kinachoendelea ndani ya ndoa ya kaka yake Ali Kiba na mkewe, baada ya kuenea uvumi kwamba wawili hao mambo si shwari.

Baadhi ya wanamitandao wanadai baada ya kuzinduliwa video ya Nandy na Alikiba, kuna sintofahamu kwenye ndoa ya kaka yake na shemeji yake.

"Siwezi kujibu suala la Ali na mke wake kwa sababu silali nao, hivyo sijajua kuna nini, ila kwenye familia hakuna tatizo kwa sababu wanajua sisi ni wanamuziki pia tushapata idhini kutoka kwa mama ingawa kunaonekana na kuhisiwa kuna matendo tofauti, kazi za mitandaoni hatuwezi kuzijaji na huwezi kumpangia mtu akujibu nini," amejibu Abdu Kiba.

## Video 'Giny Baba' yazidi kupambwa

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, ambaye anakuja kwa kasi, Joshen Adam, maarufu kama 'Giny Baba' amemaliza kazi ya kuchukua picha za video ya wimbo wake mpya.

Akizungumza na Nipashe, Meneja wa mwanamuziki huyo Yasso Boy, amesema kazi hiyo inafanywa na kampuni ya Blue Image ya jijini Dar es Salaam chini ya mtayarishaji Ibraso.

"Kazi ya uchukuaji picha za video inakamilika leo, baada ya siku kadhaa wapenzi wa muziki watashuhudia mapinduzi makubwa kutoka kwa Giny Baba ambaye hataweza kuzuilika kwani tumejipanga kutoa nyimbo mfululizo." Amesema Yasso.

Hata hivyo, amesema ngoma hiyo itazinduliwa hivi karibuni baada ya mipango yote kukamilika na kuwaomba mashabiki wa muziki kukaa tayari.



## HABARI MICHEZO

# PSG YAJIANDAA KUMSAJILI MESSI




**PARIS, Ufaransa**

LIONEL Messi ameripotiwa kwamba, bado yupo kwenye mipango ya kuwaniwa na Klabu ya Paris Saint-Germain, kwa mujibu wa ESPN.

Messi mwenye umri wa miaka 33, mkataba wake wa sasa Barcelona unamalizika mwishoni mwa msimu huu, akiwa amebakia kwenye klabu hiyo baada ya maombi yake ya kutaka kuondoka kushindikana mwanzoni mwa mwaka huu.

Huku majaliwa yake bado yakiwa hayajulikani kuendelea kukaa pale Katalunya, nyota huyo wa Barcelona anawaniwa na PSG.

Kwa mujibu wa ripoti PSG inaangalia uwezekano wa kumsajili Messi mara tu makataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu.

Pamoja na Manchester City na Inter Milan, PSG imekuwa ikiongoza kwenye mbio za kuiwania saini ya nyota huyo wa kimataifa wa Argentina.

Ripoti zinasema kwamba, Neymar na Mkurugenzi wa michezo, Leonardo wamejadiliana kuhusu kumleta Messi pale PSG.

Hiyo imekuja siku chache baada ya Neymar kusema kwamba anataka kucheza tena na Messi msimu ujao.

# ZORC ANAIMANI SANCHO ATARUDI KWENYE UBORA



**DORTMUND, Ujerumani**

JADON Sancho atamaliza wakati wake mgumu na kurudi kwenye ubora wake kwa Borussia Dortmund, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa michezo, Michael Zorc.

Baada ya kuwa na msimu wa kuvutia wa 2019-20 ambapo alifunga mabao 20 na kutoa pasi za mwisho 19 katika mechi 44, Sancho amekuwa kwenye wakati mgumu msimu huu.

Katika mechi 12, nyota huyo wa kimataifa wa England amefunga mabao matatu na kutoa pasi za mwisho nne na bado hajafunga kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Akizungumza kabla ya mchezo wa jana Jumamosi wa Dortmund dhidi ya Eintracht Frankfurt, Zorc alimtetea straika huyo.

"Naamini ni rahisi kuona kwamba hayupo kwenye ubora wake," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Naweza kusema anajaribu kujituma sana uwanjani. Anajaribu kulazimisha mambo yawe katika ubora ule anaoutaka yeye mwenyewe.

"Jadon ni mchezaji ambaye hazungumzi sana, lakini anatoka majibu dimbani. Inaweza kuwa kesho au wiki ijayo, lakini naamini anaweza kufanya lolote na kuwa bora."

# Arteta afurahia mashabiki kuruhusiwa dimbani

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesisitiza ana furaha kuona mashabiki wa Tottenham Hotspur wataruhusiwa kuingia uwanjani kwenye mchezo wa leo Jumapili kati ya miamba hao wa jiji la London.

Na akabainisha kwamba kuruhusiwa kwa mashabiki hao kwenye dimba lao la nyumbani hakuwapi wakati mgumu wao.

Washikabunduki hao watakuwa kwenye dimba la Tottenham Hotspur leo na mashabiki 2,000 wataruhusiwa kuingia uwanjani kushuhudia mchezo huo, baada ya serikali ya Uingereza kulegeza masharti ya kujikinga na virusi vya corona.

Mashabiki wa soka hawajaruhusiwa kuingia uwanjani tangu Machi mwaka huu baada ya mlipuko wa corona na sasa wataanza kurudi kwa masharti uwanjani.

Wakati mashabiki hao wakiruhusiwa kuingia uwanjani Arteta, amesema: "Ni jambo zuri kuona mashabiki wanaanza kuruhusiwa kuingia uwanjani, lakini hilo sio jambo gumu kwetu.

"Naamini uwepo wao utaongeza molari kwa wachezaji na sisi tutakuwa kwenye wakati mzuri wa kucheza kwa kujituma zaidi."

Arsenal inaingia kwenye mchezo huo ikiwa nafasi ya 14 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# IBRAHIMOVIC HANA MPANGO WA KUSTAAFU

Amekuwa na kiwango cha kuvutia tangu kuanza kwa mwaka huu, ingawa...

**MILAN, ITALIA**

NYOTA wa AC Milan, Zlatan Ibrahimovic, hana mpango wa kustaafu wakati akijihisi kuwa fiti zaidi, akisisitiza woga hautakuwa sehemu ya kufanya maamuzi hayo.

Ibrahimovic ameanza vizuri zaidi msimu huu akiwa na vinara hao wa Serie A, Milan, akifunga mabao 11 katika mechi 10, kabla ya kuumia misuli mwanzoni mwa mwezi uliopita.

Straika huyo mkongwe amekuwa na kiwango cha kuvutia kwa miamba hao wa Serie A tangu kuanza kwa mwaka huu, ingawa mzungumzo kuhusu majaliwa yake yakijadiliwa baada ya nyota huyo kufikisha umri wa miaka 39 Oktoba mwaka huu.

Lakini Ibrahimovic, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu, amesema anataka kuendelea kucheza kadili anavyoweza.

"Kwa kuwa naendelea kuwa fiti nitaendelea kucheza. Kwa sababu miaka inavyokwenda, hatuzungumzii tena kuhusu ubora, lakini ni kuhusu tu namna gani uko fiti," alisema akiiambia Sky Sport.

"Kama ukiwa fiti vya kutosha unaweza kufanya vizuri, kama (Francesco) Totti. Lakini ni jambo linalomtokea kila mmoja.

"Sio kukosekana kwa ubora, kama mtu akiwa fiti anaweza kufanya jambo lolote kwa wakati wowote.

"Hilo ndio jambo la msingi, kupoteza ubora ni kitu kisichowezekana. Ni kama vile unaweza kufanya jambo ukiwa fiti au la."

Ibrahimovic alirudi Ulaya mwanzoni mwa mwaka huu baada ya kukaa misimu miwili katika timu ya LA Galaxy inayoshiriki Ligi Kuu ya Marekani, MLS.

Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Sweden amesema atakuwa mkweli kuhusu majaliwa yake, akibainisha kuwa alikwenda Ligi Kuu ya Marekani baada ya kutojulikana kwa hatima yake kama anauweza kufanya vizuri Ulaya.

## KWA UFUPI

### DIER ALITAKA KUONDOKA SPURS
MLINZI wa Tottenham Hotspur na England, Eric Dier mwenye umri wa miaka 26, amekubali kwamba alikuwa tayari kuondoka katika klabu hiyo kabla ya kuaminiwa katika nafasi ya ulinzi wa kati. **(Mail)**

### BARNES AWANIWA MAN U
MANCHESTER United inamfikiria winga wa Leicester, Harvey Barnes mwenye umri wa miaka 22, katika dirisha la usajili lijalo badala ya Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20 kutoka Borussia Dortmund. **(Sun)**

### DIALLO MAMBO SAFI EPL
KLABU ya Manchester United ina matumaini ya kupata kibali cha kazi kwa winga wa Atalanta raia wa Ivory Coast, Amad Diallo mwenye umri wa miaka 18 ambaye anaweza kujiunga nao wakati wa dirisha dogo la Januari. **(Manchester Evening News)**

### INGS NA MKATABA MPYA
STRAIKA wa England, Danny Ings mwenye umri wa miaka 28, ameshauriwa kusaini mkataba mpya wa muda mrefu na klabu yake hiyo na kocha wake, Ralph Hasenhuttl, ambapo mkataba wake wa sasa umebakiwa na miezi 18. **(Sky Sports)**

### MOYES KUJIFUNGA WEST HAM
KLABU ya West Ham ipo tayari kumpa mkataba wa muda mrefu, kocha wake wa sasa, David Moyes. **(Times, subscription required)**

### SOLSKJAER ATAKA USAJILI
KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amekataa madai kwamba, timu yake haina kiwango cha kuvutia na amesisitiza usajili mpya utakisaidia kikosi hicho kuwa bora. **(Sky Sports)**

### TUCHEL KUTUA MAN U
MANCHESTER United inaweza kumchukua kocha wa Paris St-Germain, Thomas Tuchel kama Ole Gunnar Solskjaer atafukuzwa wiki ijayo. **(Bild)**

### WINKS KUONDOKA SPURS
KIUNGO wa Tottenham Hotspur, Harry Winks mwenye umri wa miaka 24, anaweza kutaka kuondoka wakati wa dirisha la Januari ili kupata nafasi ya kucheza zaidi. **(Mirror)**

### ROSA AWANIWA MAN CITY
MANCHESTER City inapanga kumsajili kiungo wa Gremio, Diego Rosa mwenye umri wa miaka 18 raia wa Brazil. **(Manchester Evening News)**

### BISSOUMA KUMRITHI WIJNALDUM
KIUNGO wa Brighton, Yves Bissouma mwenye umri wa miaka 24, ni moja ya majina yanayotajwa kurithi mikoba ya Georginio Wijnaldum pale Liverpool mwenye umri wa miaka 30, ambaye amekuwa akihusishwa na Barcelona. **(Liverpool Echo)**

### OZCAN KUTUA ARSENAL
ARSENAL imefufua mipango yake ya kutaka kumsajili kiungo wa Istanbul Basaksehir, Berkay Ozcan mwenye umri wa miaka 22 raia wa Uturiki. **(Transfermarkt)**



HABARI MICHEZO

# KIPA WA BIASHARA ANUKIA AZAM FC

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI dirisha dogo la usajili wa Ligi Kuu Tanzania Bara likitarajiwa kufunguliwa, kipa namba moja wa Biashara United, Daniel Mgore anatajwa kuwaniwa na Azam FC kwenda kumsaidia David Kissu.

Mgore, ambaye ni kipa namba moja wa Biashara, inadaiwa anahitajiwa kwa udi na uvumba na Azam, huku Mwenyekiti wa Biashara, Selemani Mataso akisema kuwa hao hawana tatizo na hilo, ili mradi tu taratibu zifuatwe.

"Hizi nadhani bado ni tetesi kwa sababu hatujafuatwa kama uongozi, lakini ikiwa wanahitaji saini ya mchezaji wetu hatuna tatizo, tunaweza kuzungumza na kufikia makubaliano kwa sababu hata sisi wenyewe huwa tunachukua wachezaji kutoka klabu zingine," alisema mwenyekiti huyo.

Ofisa Habari za Azam, Thabit Zacharia, amesema kuwa suala la usajili kwenye kikosi chao liko mikononi mwa kocha na si vinginevyo. Azam imemchukua kocha George Lwandamina kuchukua mikoba ya Aristica Cioaba ambaye alitimuliwa baada ya timu kutofanya vizuri.

"Ni kweli kuna mahitaji ya wachezaji na tutasajili kipindi cha dirisha dogo, lakini hii itategemea na ripoti ya mwalimu wetu baada ya kukaa na kikosi atajua ni wapi kwenye mapungufu na atatoa mapendekezo yake," alisema msemaji huyo.

Mgore ni mmoja wa makipa ambao wanakuja juu kwa sasa kutokana na kiwango chake bora anachoendelea kuonyesha kiasi cha kuwatoa udenda klabu kubwa kutaka kumchukua.

Kipa huyo alihusishwa pia kwenda Simba kumsaidia Aishi Manula. Kipindi cha dirisha dogo la usajili linatarajiwa kufunguliwa Desemba 15 kwa klabu kutakiwa kusajili wachezaji kutoka ndani na nje ya nchi ambao wanaona wanafaa kwa ajili ya kuziba upungufu uliyojitokeza kwenye mechi za mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi St Mary's Tabata, wakiwaburudisha wageni kwa nyimbo za wasanii wa kizazi kipya katika mahafali ya wanafunzi wa shule ya awali Tabata jijini Dar es Salaam. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Kocha KMC atoa siri ushindi

**Na Saada Akida**

BAADA ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Dodoma FC, Kocha wa KMC, Habib Kondo, amesema alitumia dakika 45 ya kipindi cha kwanza kuwasoma wapinzani wake hao na kupata pointi tatu katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kondo alisema hawakuwahi kuwaona wapinzani wake hao wakicheza hivyo aliwaheshimu na kucheza kwa tahadhari kubwa.

Alisema kipindi cha kwanza alikuwa makini na kuwasisitiza wachezaji wake kutulia na kipindi cha pili wakafanikiwa kupata nafasi nyingi za wazi licha ya kufunga bao moja tu.

"Malengo yetu ni kutafuta pointi tatu muhimu, Dodoma ni timu nzuri pia wageni katika ligi, sijawahi kuwaona wakicheza hivyo niliwaeleza wachezaji wangu kucheza kwa tahadhari na kuwaheshimu wapinzani wetu, na hilo imetusaidia kupata ushindi huo," alisema Kondo.

Alisema kipindi cha pili walifanikiwa kuwasoma na kujua mbinu za wapinzani wako hao na kufanikiwa kutengeneza nafasi ya wazi na kushindwa kuzitumia kutokana na kutokuwa na utulivu wa washambuliaji wangu.

Kocha huyo alisema baada ya mechi hiyo wanaenda kufanyia kazi upungufu uliyojitokeza katika mechi hiyo ili yasijirudie katika mechi zetu zijazo za ligi hii.

## Dodoma yajipanga upya Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

BENCHI la ufundi wa timu ya Dodoma FC, limesema kikosi chake ni kigeni katika Ligi Kuu Tanzania Bara na kinahitaji muda wa kujipanga zaidi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi, Retunus Shija, alisema licha ya kutopata matokeo mazuri kwa mechi za hivi karibuni, lakini anaimani watafanya vizuri kwa michezo iliyopo mbele yao.

Alisema timu yao bado mpya katika ligi hivyo wanajaribu kufanyia kazi upungufu wao kwa ajili ya mechi zao zijazo.

"Kupoteza mechi mmoja au mbili mfululizo haimaanishi tuko katika nafasi mbaya kwenye ligi. Ndio kwanza mzunguko wa kwanza huu, tutatumia muda huu kuimarisha kikosi chetu katika matatizo ambayo yamejitokeza," alisema Shija.

Alisema ameona upungufu wa timu yao kuhakikisha mechi zijazo watafanya vizuri na kuendelea kubaki katika mikikimikiki ya ligi hiyo.

"Tunaenda kufanyia kazi upungufu wa kikosi chetu kwa ajili mechi zetu zijazo hasa safu ya ushambuliaji kuwa makini," alisema.

Dodoma inashika nafasi ya 10 baada ya kujikusanyia pointi 16 katika michezo 13 ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

## GSM yaja na shindano la ung'arishe nyumba

**Na Saada Akida**

KAMPUNI ya uuzaji wa samani za nyumba, ofisi na mavazi ya GSM, imezindua shindano jipya la Shinda na ung'arishe nyumba yako' pamoja na safari ya kwenda kutalii katika hifadhi ya Ngorongoro kwa wateja wao ambalo limeanza Desemba Moi mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Biashara Mkuu wa GSM, Allan Chonjo, alisema wamewapa nafasi wateja na wadau wao kujishindia samani pamoja na nguo mbalimbali katika msimu wa sikukuku za mwisho wa mwaka.

Alisema lengo kubwa la kuanzisha shindano hilo ni kuwapa nafasi wateja wao wote, kununua samani za kampuni hiyo ili kujishindia zawadi kabambe watakazofurahia.

"Mwaka 2020 umekuwa na changamoto nyingi hususani mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19, ambao uliathiri shughuli mbalimbali za kijimii na hata kuharibu mipango na malengo, kwa kulitambua hilo sisi GSM tukaona hatua budi kuanzisha shindano hili ili kila mmoja aweze kupata nafasi ya kujishindia bidhaa aliyokuwa akiitamani kutoka katima kampuni yetu," alisema Chonjo.

Alisema shindano hilo litahusisha kwa maana ya GSM Home ambao wauzaji wa samani za nyumbani na ofisini pamoja na Rtail ambao ni wauzaji wa mavazi chini ya chapa SPLASH, Babyshop.

"Kwa upande wa mavazi mteja akinunua nguo za thamani ya zaidi ya Sh. 50,000 kwa mara moja atangia kwenye droo ya kujipatia zawadi mbalimbali zikiwamo vocha za thamani ya Sh. 250,000 au zawadi kubwa ya kulipiwa safari ya kwenda kutalii mbuga ya Ngorongoro kwa watu wawili," alisema Chonjo.

# Michezo

Jumapili Desemba 6, 2020

Nipashe





Ibrahimovic hana mpango wa kustaafu

HABARI UK 22


## Yanga kazi kazi kwa Ruvu Shooting leo

**Na Adam Fungamwango**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara Yanga, leo saa 1:00 usiku watakuwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kuwavaa Ruvu Shooting kwenye mechi ya raundi ya 14 ya Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea.

Yanga inayoongoza ligi kwa pointi 31, ikiwa imecheza mechi 13, inatarajiwa kuivaa Ruvu Shooting inayofundishwa na kocha wao wa zamani, Charles Boniface Mkwasa.

Litakuwa ni pambano kali kwa timu zote, huku Yanga ikitakiwa kuwa na tahadhari kwani Ruvu Shooting imejinasibu kuiadhibu timu hiyo kama ilivyofanya kwa wakani zao wa jadi, Simba ilivyowachapa bao 1-0 Oktoba 26 mwaka huu kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Pia inatakiwa kuwa makini na mastraika wawili hatari, Abdulrahman Mussa na Fully Maganga ambao huwa hawatabiriki.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Cedric Kaze amesema kuwa anatambua shauku ya mashabiki wa klabu hiyo ni kutwaa ubingwa iliyoukosa kwa muda mrefu jambo ambalo analipambania.

"Furaha ya mashabiki na viongozi na kuona tunatwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara, ila bado tuna kazi ya kufanya kwa kuwa ushindani ni mkubwa kwenye ligi hii, ila ni lazima tupambane," alisema kuelekea kwenye mechi ya leo.

Yanga ndiyo timu pekee kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo haijapoteza mechi yoyote mpaka sasa, ikiwa imeshinda mechi tisa na kutoka sare nne kwa mechi 13 ambazo imecheza.

Pia katika mechi ya leo, wanachama na mashabiki wa Yanga watapata nafasi ya kuona mchezaji wao mpya, Mrundi Saido Ntibanzokiza ambaye tayari amejiunga na timu hiyo, lakini kwa sasa anasubiri kipindi cha dirisha dogo ndipo aanze kufanya vitu vyake.

Leo watapata nafasi ya kumuona, kusalimia naye, ikiwezekana kupiga naye picha tu.

Kwa upande wa Ruvu Shooting, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Masau Bwire amesema kuwa katika mechi ya leo hakuna utani, watafanya kweli ili kupata pointi tatu na kuishusha Simba kwenye nafasi ya tatu. Simba na Ruvu Shooting zote zina pointi 23, hivyo maafande hao wanahitaji sare au ushindi ili kuiengua timu hiyo kwenye nafasi hiyo.

"Tunaingia uwanjani tukiwa na hesabu za kupata pointi tatu, mashabiki wajitokeze kwa wingi kutushangilia ili tufanye kama tulivyofanya kwa Simba," alisema Masau.




Mchezaji wa Simba, Mzamuru Yassin, akiwapiga chenga wachezaji wa Plateau wakati wa mchezo baina ya timu hizo, uliopigwa jana Uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SIMBA YATAKATA LIGI YA MABINGWA

## Sasa kukutana na Platinum ya Zimbabwe...

**Na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika Simba, jana ilitinga raundi ya kwanza ya michuano hiyo, baada ya kutoka suluhu na Plateau United ya Nigeria.

Mechi hiyo kali na ya kusisimua iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam.

Simba imefanikiwa kusonga mbele kwenye michuano hiyo baada ya kushinda ugenini bao 1-0 nchini Nigeria wiki moja iliyopita, hivyo matokeo ya jumla yanabaki ni bao hilo.

Kwa matokeo hayo, Simba itacheza na Platinum ambayo imefanikiwa kusonga mbele jana, kwenye michuano hiyo kwa kuifunga Costa do Sol ya Msumbiji mabao 2-0 nchini Zimbabwe.

Ikiwa ugenini wiki moja iliyopita, Platinum pia ilishinda mabao 2-1, hivyo inasonga mbele ya jumla ya mabao 4-1.

Kama ilivyotarajiwa ulikuwa mchezo mgumu kwa pande zote mbili, licha ya kwanza ulianza taratibu kama vile timu zote zilikuwa zinasomana.

Dakika ya tisa tu, Jonas Mkude alipiga shuti kali lililotoka nje ya lango, huku kwenye dakika ya 14, Mzamiru Yassin alipewa pasi ya kisigino kutoka kwa John Bocco, lakini alipiga shuti juu la lango la Plateau United.

Wanaigeria walifanya shambulizi kali langoni mwa Simba dakika ya 23, lakini krosi ya Gabriel Wassa ilitua kwenye kichwa cha Issa Ndala ambaye alipiga kichwa dhaifu kilichodakwa na kipa Aishi Manula.

Nusura Plateau United ipate bao dakika ya 35, baada ya mabeki wa Simba kuzembea kumkaba Ibrahim Buhari ambaye aliachia shuti lililodakwa na kipa Manula.

Luis aliikosesha Simba bao dakika ya 38, baada ya kubaki na kipa Adam Aboubakar, lakini shuti lake lilipanguliwa na kipa huyo na baadaye kuudaka tena.

Kipindi cha pili, Plateau walibadilika. Wakaanza kucheza mpira wa kasi na kufanya mashambulizi kadhaa langoni mwa Simba, lakini mabeki Paschal Wawa na Erasto Nyoni walikaa imara kuokoa hatari, wakisaidia na Shomari Kapombe na Mohamed Hussein 'Tshabalala'.

Dakika ya 66, Hassan Dilunga alikokota mpira umbali mrefu na kubaki na kipa Adam, lakini shuti lake lilimbabatiza kipa huyo kabla ya kuokolewa na mabeki.

Bernard Morrison aliyeingia badala yake Dilunga, alipiga shuti lililopanguliwa na kipa dakika ya 78, na hiyo ilikuwa ni kabla ya Luis Miquissone aliyesumbua mno ngome ya Wanaigeria hao kukosa bao dakika ya 74.

Hali ingeweza kubadilika dakika 88 na dakika za nyongeza, wakati Plateau walipokosa mabao mawili ya wazi kupitia kwa Ibrahim Buhari alipiga shuti lililotoka nje kidogo ya lango na Uchoweche Oche aliyemchungulia Manula akiwa ametoka kidogo golini alipiga mpira wa juu ambao almanusura utinge wavuni, lakini ukatoka sentimeta chache na kuinusuru Simba kwenda kwenye matuta.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042